**WATANO** kunyongwa hadi kufa kosa la mauaji ushirikina

UKURASA 3



**AUAWA** pembeni wakutwa ujumbe 'mke wa mtu sumu'

UKURASA 7


ama
AFYA NA MAZINGIRA
NDIVYO KILIVYO KIINI CHA WATOTO VICHWA VIKUBWA, MGONGO WAZI
KITENDAWILI CHA DAWA MIFUGO KUTIBU CORONA
PARFAIT KOLELAS
**Mpinzani mkuu wa Rais Sassou Nguesso aliyefariki kwa corona siku kabla kura**

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Aprili 1, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580537

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


# ZEGE HALILALI

**RAIS** afumua Baraza la Mawaziri, aonya chuki na kutowajibika, ateua Katibu Mkuu Kiongozi...

*Endelea Ukurasa 2*



Katibu Mkuu Kiongozi, Hussein Kattanga



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mohammed Mchengelwa



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Masauni



Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk






Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Hamis Juma akimwapisha Dk. Philip Isdor Mpango kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma jana. **Picha zaidi ukurasa wa 2 na 18. PICHA: IKULU**

## Shamim, mumewe wafungwa maisha

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA SC, YANGA KURUDIANA MEI 8** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**

HABARI KITAIFA



Rais Samia Suluhu Hassan akiagana na Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa pamoja na Spika wa Bunge, Job Ndugai, baada ya hafla ya uapisho wa Makamu wa Rais, Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Samia: Zege halilali

**Augusta Njoji na Romana Mallya**

ZEGE hailali! Ndiyo inavyoonekana kwenye serikali ya Rais wa sita, Samia Suluhu Hassan, ambaye baada ya jana kuapishwa kwa Makamu wake, Dk. Philip Mpango, alitangaza mabadiliko ya Baraza lake la Mawaziri.

Baraza hilo ni lenye mabadiliko madogo ya lile la awali chini ya Rais wa tano, Hayati Dk. John Magufuli kutokana na kuteua wapya ambao wawili amewapa uwaziri na wengine kubadilishwa wizara. Wakati hayo yakifanyika, Rais Samia amemteua Balozi wa Tanzania nchini Japan, Hussein Kattanga, kuchukua nafasi ya aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Bashiru Ally, ambaye ameteuliwa kuwa Mbunge.

"Nimesema kuondoka kwa Dk. Mpango kumeacha nafasi ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango na tuko kwenye Bunge la Bajeti ambalo Waziri wa Fedha ni muhimu kuwapo.

"Nimesema nisifanye kazi kidogo kidogo hii imenipa nafasi ya kulitizama upya Baraza la Mawaziri, nimefanya mabadiliko madogo ndani ya Baraza la Mawaziri. Zege halilali wanasema ni hapa hapa," alisema. Alisema kabla ya kuunda baraza amefanya uteuzi wa wabunge watatu ambao ni Dk. Bashiru, Balozi Liberata Mulamula na Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk.

"Uteuzi huu umenipelekea (umenifanya) kufanya Baraza la Mawaziri kama ifuatavyo Ofisi ya Rais... naomba mtulie viroho visinanii, manake nimeona nyuso zimeshabadilika vifua vinapiga vikubwa hivi hivi (mapigo ya moyo)" alisema na kuanza kutaja mawaziri na manaibu.

Akitaja baraza lake jipya la mawaziri jana Ikulu, Chamwino jijini Dodoma, Rais Samia alisema ameona awabadilishe kutoka wizara moja kwenda nyingine kwa sababu tangu walipoapa hadi sasa ni muda mfupi kuona nani kashindwa na nani kafanya nini.

"Niwaombe sana mkafanye kazi zenu kila mmoja kwa wizara yake na mahali pake mkafanye kazi. Alivyosema Hayati Dk. John Magufuli, Manaibu Mawaziri wakatumike vizuri, mna mtindo huwa hamuwapangii kazi, kuna kudharauliana na hata sasa nina baadhi ya kesi.

"Nimesema tunaanza, dharau zikiendelea basi tutajua cha kufanya huko mbeleni, ninachotaka ni kazi na sitaki kusikia jambo lingine, naomba mkachape kazi."

**WALIOBADILISHWA**

Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ni Ummy Mwalimu, ambaye awali alikuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira na Manaibu Waziri wamebaki ambao ni Dk. Festo Ndugange na David Silinde.

**MAWAZIRI WAPYA**

Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora aliyeteuliwa ni Mohamed Mchengerwa na Manaibu Waziri wamebaki Deogratius Ndejembi na Mwita Waitara.

Wizara ya Fedha na Mipango, ameteuliwa Mwigulu Nchemba na naibu wake ni Hamad Yussuf Masauni huku Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki akiteuliwa Balozi Liberata Mulamula na Naibu Waziri ni Mbarouk Nassor Mbarouk.

**WALIOHAMISHWA**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Kazi Maalum) anakuwa George Mkuchika ambaye awali na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora na Ofisi ya Makamu wa Rais anakuwa Suleiman Jafo ambaye awali alikuwa TAMISEMI na Naibu Waziri ni Hamad Chande.

Aidha, Rais Samia ameiondoa Wizara ya Uwekezaji kutoka Ofisi ya Rais kwenda ofisi ya Waziri Mkuu na sasa itakuwa chini ya Waziri Geoffrey Mwambe ambaye awali alikuwa Waziri wa Viwanda na Biashara huku Naibu Waziri ni Wiliam Ole Nasha.

Rais Samia amewapa miezi mitatu kuhakikisha wizara hiyo mpya iwe imeunda na kuanza kazi haraka na kuwaeleza kuwa vinginevyo watamuonyesha hawajui cha kufanya.

Wizara ya Katiba na Sheria, Waziri ni Palamagamba Kabudi na Naibu Waziri ni Geofrey Pinda.

**WIZARA AMBAZO HAZIJAGUSWA**

Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi na Ulemavu, Jenister Mhagama na Manaibu wake Patrobas Katambi na Ummy Nderiananga wakati Wizara ya Ulinzi na Kujenga Taifa ni Elias Kuandikwa. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni George Simbachawene na Naibu wake, Khamis Hamza Chilo.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamliho na Naibu Waziri ni Msongwe Kasekenya wakati Wizara ya Madini ni Dotto Biteko na Naibu Waziri, Prof. Shukuru Manya.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi na Naibu Waziri, Dk. Angelina Mabula na Wizara ya Maji, Juma Aweso na Naibu Waziri ni Maryprisca Mahundi. Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa na Naibu amembadilisha na kuwa, Pauline Gekul.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako na naibu wake ni Kipanga Juma Omary. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dorothy Gwajima na Naibu Waziri, Dk. Godwin Mollel na Mwanaidi Ally Khamis ambaye atashughulikia masuala ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto.

Wizara ya Nishati, Waziri, Dk. Medad Kalemani na naibu wake ni Stephen Byabato. Wizara ya Utalii, Dk. Damas Ndumbalo na Naibu Waziri ni Mary Masanja. Wizara ya Kilimo, Prof. Aldolf Mkenda na Naibu Waziri ni Hussein Bashe. Wakati Wizara ya Mawasiliano Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile na Naibu Waziri ni Kundo Matthew.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, waziri ni Mashimba Ndaki na Naibu Waziri ni Abdallah Ulega kutoka Wizara ya Michezo.

# ... Aanika kilichombeba Mpango

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametaja kilichombeba Dk. Philip Mpango kuwa Makamu wa Rais wa Tanzania huku akibainisha mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na mchumi huyo kutokuwa na "hili wala lile".

Katika hotuba yake baada ya Dk. Mpango kuapishwa kushika madaraka hayo makubwa jana Ikulu Chamwino, Dodoma, Rais Samia alisema, mbali na kutokuwa na 'hili wala lile', Dk. Mpango ni mchumi mahiri, mchapakazi na mcha Mungu.

"Mheshimiwa Mpango hongera sana kwa kutwikwa madaraka katika ngazi nyingine kwenye nafasi hii. Nilizunguka sana kutafuta nani awe, nilipata salamu nyingi sana. Nikaangalia ndani na nje ya Bunge, lakini nikarudi ndani ya Bunge. "Na mtu niliyemwona kwa sasa hivi anafaa kwenda na mimi, ni ndugu yetu Philip, jina la katikati sijui kulitamka vizuri, lakini ninadhani nilivutika na jina Mpango pia.

"Lakini mbali ya jina Mpango, Philip ni mcha Mungu, Philip ni mchumi mahiri, ni mchapakazi, mzoefu na hodari. Lakini Philip pia ametulia, hana hili wale lile.

"Majina mengine niliyokuwa nayo yalikuwa yana hili, yana lile, yana mbele, lakini Philip nilikuta katulia. Kwa hiyo, nikasema huyu ananifaa kwenda naye. Hongera sana," Rais Samia alisifu.

Rais alisema mbali na majukumu yake yaliyowekwa kikatiba, Dk. Mpango atamsaidia kwenye masuala ya kiuchumi na udhibiti wa matumizi ya fedha za serikali.

Aliweka wazi kuwa vikwazo vingi vya Muungano vilivyokuwapo, vimeshatatuliwa na kilichokuwa kimebaki, kilikuwa kimekaliwa na Wizara ya Fedha na Mipango, ambayo Dk. Philip Mpango alikuwa kiongozi wake, hivyo akamtaka Makamu wa Rais mpya huyo kuwasaka aliowaita wanga wa kero hiyo na kumalizana nao kwa kuwa "mwanga mpe mtoto wako akulelee".

**MPANGO: SAMIA NITUME**

Baada ya kula kiapo, Dk. Mpango alipata nafasi ya kuzungumza, akimwambia Rais Samia kuwa yuko tayari kupangiwa majukumu na Mkuu wa Nchi huyo usiku na mchana na atakuwa mtiifu na mnyenyekevu kwake.

"Sikuota na wala sikutegemea kwamba mimi mtoto wa maskini kutoka Buhigwe ningeteuliwa kushika nafasi hii. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Rais.

"Ninakuahidi sitakuwa kama yule Yuda aliyemsaliti Yesu. Sasa nitume kazi mchana na usiku, nitatekeleza yaliyoko katika ilani yetu ya chama na maono yako," Dk. Mpango alisema na kutoa ujumbe kwa wananchi wa majimbo ya Buhigwe na Muhambwe mkoani Kigoma, akiwaomba kuwachagua wagombea watakaopendekezwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) wakati wa uchaguzi mdogo unaofuata.

Awali, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, alimhakikishia Dk. Mpango kuwa serikali yake itampa ushirikiano mkubwa katika majukumu yake mpya, huku akiweka matumaini makubwa kumalizwa kwa kero za Muungano zilizobaki chini ya uongozi wa mtaalamu huyo wa uchumi.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, alimshukuru Rais Samia kwa kulipaisha Bunge kwa kupendekeza Makamu wa Rais atoke miongoni mwa wabunge wake, huku akimkaribisha Mkuu wa Nchi bungeni na kumwaahidi ushirikiano mkubwa.

Spika Ndugai pia alimwomba Rais kuteua Waziri wa Fedha na Mipango mapema ili kutokwamisha shughuli za Bunge la Bajeti linaloendelea mjini Dodoma na ombi lake hilo halikuchukua zaidi ya nusu saa likapatiwa majibu.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, alisema mahakama itaendeleza ushirikiano mzuri kati yake na Dk. Mpango uliokuwapo kipindi cha uongozi wake Wizara ya Fedha na Mipango.

Aliwakumbusha wananchi na viongozi kuheshimu sheria za nchi, akisisitiza kuwa sheria hazina matatizo, bali matatizo yako kwa binadamu na kuonya kuwa sheria zikitumika vibaya, ni hatari kwa ustawi wa nchi.

## HABARI KITAIFA



Waombolezaji wakiaga mwili wa Mtangazaji wa ITV/Radio One, marehemu Blandina Sembu, wakati wa ibada iliyofanyika kwenye Kanisa la Katoliki lililopo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Shamim na mumewe wafungwa maisha

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Uhujumu Uchumi na Rushwa maarufu kama mafisadi imewahukumu kifungo cha maisha, Mwandishi wa Habari Shamim Mwasha (41) na mumewe Abdul Nsembo (45) baada ya kukutwa na hatia ya kusafirisha na kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya aina ya heroine gramu 232.70.

Mahakama hiyo pia imetaifisha mali zote za washtakiwa kuwa za serikali.

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Jaji Elinaza Luvanda, ambaye alisema baada ya ushahidi wa Jamhuri bila kuacha shaka Mahakama imejiridhisha na kuthibitisha mashtaka dhidi ya Nsembo na mkewe pasipo kuacha shaka yoyote.

Kabla ya kuwasomea hukumu hiyo, Jaji Luvanda aliwasomea maelezo ya shauri hilo na kutupilia mbali hoja kadhaa zilizotolewa na upande utetezi wakati wa kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili.

Katika maelezo hayo, Jaji Luvanda alisema kuwa hoja za majumuisho ya shauri hilo pande zote mbili zilitoa maelezo yake na upande wa utetezi ulipingana na mambo kadhaa katika ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri.

"Katika hoja za majumuisho pande zote mbili ziliwasilisha majumuisho yake, hakukua na ubishani kuwa washtakiwa wote waliishi katika nyumba moja, hakukuwa na ubishani gari aina ya Land Rover Discovery yenye namba T 817 DQN, ambalo liliwasilishwa kama kielelezo mahakamani ni mali ya mshtakiwa namba moja, lakini gari hiyo na nyumba vilihusishwa katika upekuzi," alisema Jaji Luvanda.

Pia alisema katika ushahidi ilielezwa kuwa wakati wa upelelezi chumbani kwa washtakiwa vilikutwa vikopo vinne vyenye unga na baadaye kwenye gari ulikutwa mfuko wa kitambaa cheupe uliofungwa kwa nailoni angavu wenye unga ndani yake.

Katika ushahidi wa Nsembo, alisema kuwa upekuzi haukuwa na mpangilio kwa kuwa askari walikuwa wakitoka na kuingia huku zoezi la upekuzi likiendelea, hoja iliyoonyesha kuwa huenda vielelezo viliwasilishwa mahakamani vilikuwa vya kupandikiza.

"Katika hoja hiyo washtakiwa walijaribu kujenga hoja kuwa vitu hivyo vilipandikizwa, hata hivyo hawakuweka bayana ni nani na nani walikuwa wakiingia na kutoka pamoja na kuwa Abdul alikiri kuona begi lenye vitu hivyo katika ofisi za Tume ya Dawa za Kulevya. Mimi naona hoja hiyo haina mashiko," alisema.

Pia alisema Shamim alikana hakukuwa na kitu kilichokutwa katika nyumba hiyo wakati wa upekuzi na yeye alishuka chini kubembeleza watoto, ingawa alikiri kuwa vikopo vilikutwa bafuni kwake na akaeleza kuwa vilikuwa ni vipodozi.

"Kwa hiyo suala lililobaki lilikuwa ni je, mfuko mweupe uliofungwa kwa nailoni ulikutwa kwenye gari? Na kikopo kilikutwa bafuni? Maswali hayo yote yalijibiwa katika ushahidi uliotolewa na mashahidi wa upande wa Jamhuri na kuthibitishwa," alisema.

Kadhalika, Jaji Luvanda alitupilia mbali hoja ya kulikuwa na shaka katika uwasilishaji wa vielelezo kutokana na vielelezo vyote vilioneshwa mbele ya Mahakama tofauti na hoja ya upande wa utetezi kuwa ni bahasha pekee ndiyo ziliwasilishwa mahakamani.

Hoja nyingine iliyopuuzwa ni pamoja na ile ya ukiukwaji katika zoezi la upekuzi na Jaji Luvanda alisema hakukuwa na vifungu vya sheria vilivyonukuliwa na hoja ya kukatika kwa mnyororo wa uhifadhi wa vielelezo ambayo alisema haina mashiko na baadaye aliwatia hatiani.

"Baada ya kueleza haya hadidu ya kwanza imejibiwa kunye vielelezo vyote vilivyokutwa nyumbani kwa washtakiwa, hivyo washtakiwa wote mmekutwa na hatia, Mahakama inawatia hatiani," alisema.

Baada ya kuwatia hatiani upande wa Jamhuri uliomba Mahakama itoe adhabu kulingana na sheria inavyoagiza kwa sababu kosa walilofanya linaleta madhara makubwa kwa jamii ikiwamo utegemezi na upungufu wa afya ya akili.

Mawakili wa utetezi, Juma Nassoro na Hajra Mungula, waliomba huruma ya Mahakama kwa kuzingatia kuwa washtakiwa hao ambao ni wanandoa ni wazazi wa watoto watatu wanaohitaji malezi ya wazazi na kuiomba Mahakama itoe hukumu kwa kuangalia huruma hiyo hasa ikizingatia kuwa washtakiwa ni wakosaji kwa mara ya kwanza.

Akitoa adhabu hiyo Jaji Luvanda alisema anatoa hukumu hiyo kulingana na matakwa ya sheria, na haitatoa mwanya kwa Mahakama kutoa hukumu kwa kuangalia huruma.

"Ni kweli washtakiwa ni wakosaji kwa mara ya kwanza, lakini sheria inatoa adhabu kwa makosa haya na kwa kuwa sheria haijatoa mwanya kwa mahakama kutoa huruma nina wahukumu kifungo cha maisha gerezani kwa kosa la kwanza, na kifungo cha maisha kwa kosa la pili, pia vielelezo ikiwamo gari vinataifishwa na vile vinavyopaswa kuteketezwa mahakama inatoa amri ya kuviteketeza," alisema.

Upande wa utetezi katika kesi hiyo umeieleza mahakama nia yao ya kukata rufani huku wakiomba wapatiwe nakala ya hukumu haraka kwa ajili ya kuanza maombi.

Katika kesi hiyo Shamim ambaye ni mmiliki wa blogu ya 8020fashion na mumewe mfanyabiashara, walikuwa wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi yenye mashtaka mawili ya kusafirisha na kujihusisha na dawa za kulevya aina ya Heroine zenye uzito wa gramu 232.70 na kukamatwa Mei 1, 2019 katika eneo la Mbezi Beach, mkoani Dar es Salaam.

Baada ya hukumu hiyo vilio na simanzi vilitawala huku mshtakiwa Shamim akilia kwa uchungu.

# Wahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa mauaji kisa imani za ushirikina

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU watano wamehukumiwa kunyongwa hadi kufa baada ya kupatikana na hatia ya kumuua mkazi wa kijiji cha Usalule mkoani Njombe, Alice Mtokoma.

Waliohukumiwa adhabu hiyo ni James Msumule, Emmanuel Ngailo, Izack Ngailo, Anitha Mbwilo na Upendo Mligo.

Mawakili wa Serikali Andrew Mandwa na Matiko Nyangelo katika kikao cha mahakama kuu kilichofanyika mjini hapa mbele ya Jaji Firmin Matogolo, walidai kuwa Mei 12, 2012 washtakiwa walimuua kwa kumpiga Alice Mtokoma kwa kitu chenye ncha kali kosa ambalo ni kinyume na kifungu cha sheria na 196 na 197 cha Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 marejeo ya 2019.

Wakili Matiko Nyangelo alidai kuwa siku ya tukio, washtakiwa walimfuata nyumbani kwake Mtokoma na kumweleza kuwa kuna sehemu wanatakiwa kwenda ndipo walipofanya mauaji hayo.

Alidai kuwa chanzo cha washtakiwa hao kutekeleza mauaji hayo ni kwamba mume wa Upendo Mligo, ambaye ni mtoto wa Anitha Mbwilo, alifariki dunia ndipo wawili hao wakaenda kwa kwa mganga ili kubaini chanzo cha kifo cha kijana wao. Baada ya kwenda kwa mganga, alidai kuwa waliambiwa kuwa aliyemuua kijana wao ni Mtokoma ambaye alikuwa mke mwenzie na mshtakiwa Anitha Mbwilo.

"Baada ya kupewa maelezo hayo ya mganga, Anitha na Upendo walikula njama ya kutafuta watu ili kumuua Alice Mtokoma," alidai Matiko.

Alidai kuwa Upendo Mligo na Anitha Mbwilo waliwatafuta washtakiwa wengine, James Msumule, Emmanuel Ngailo na Izack Ngailo na kuwapa Sh. 300,000 ili wafanye mauaji hayo.

Kutokana na kosa hilo walilotenda, Jaji Matogolo aliwahukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa kwa kufuata kifungu 197 cha kanuni ya adhabu sura 16 marejeo ya 2019, ikisomwa pamoja na kifungu 322 (1)(2) cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai sura ya 20 marejeo ya 2019.


**KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ**

**EMMANUEL ANOSISYE MWAKISILWA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 581 BYG.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/174276/2021.

**TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI YA NYAMAIGA FOOD AND GENERAL SUPPLIES LIMITED**

Wamiliki wa Kampuni yenye Usajili namba (140796050) ya tarehe 13 January, 2020

Wanapenda kuwatangazia umma kwamba imekusudia kufunga Kampuni mwaka huu 2021

**MKURUGENZI**
**JOSEPH KITOKELEZI SEMUNGURUKA**

**PUBLIC NOTICE**

Kindly note that the company **"_BARRICK GROUP_"** and the employment opportunities advertised are **NOT AFFILIATED** with Barrick Gold Corporation in any way.

# Mbunge aibua tena hoja ya Katiba mpya

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Konde, Khatib Said Haji (ACT-Wazalendo), ameibua mjadala wa suala la Katiba Mpya na kuitaka serikali kumalizia mchakato huo, huku akitahadharisha kuwa kutoumalizia ni kutengeneza hasara ya mabilioni ya shilingi.

Khatib aliliibua suala hilo bungeni jijini Dodoma juzi jioni wakati wa mjadala wa maazimio ya kumpongeza Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Rais wa Tanzania na kuuenzi mchango wa Hayati Rais John Magufuli kwa utumishi uliotukuka.

Khatib alikumbusha kuwa Rais Samia alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba, hivyo ni vyema akaumalizia mchakato huo ili kuepuka hasara ya mabilioni ya shilingi.

"Katiba Mpya si matakwa ya vyama vya upinzani. Ni matakwa ya wananchi. Rais wetu wa sasa, Mama Samia Suluhu Hassan, alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba, anajua mchakato ulipoishia.

"Wakati tunampongeza hapa, tutumie pia fursa hii kumkumbusha kumalizia mchakato wa Katiba Mpya. Tumeshakula ng'ombe mzima, tunashindwa nini kumalizia mkia?

"Mchakato wa Katiba kutoendelezwa ni hasara kubwa kwa nchi. Ni hasara ya mabilioni," Khatib alionya na kuwataka Watanzania aliodai wamelazimika kukimbilia ughaibuni miaka ya karibuni, warejee nyumbani kuungana na Rais mpya, Samia kusaka maendeleo ya nchi kwa vile "nyumbani kumenoga".

Inadaiwa kuwa, iwapo mchakato huo wa kupata Katiba Mpya hautaendelezwa, taifa litapata hasara kubwa ya zaidi ya Sh. bilioni 120.

Kiasi hicho cha fedha zitakazopotea bure, kinatokana na makadirio ya jumla ya fedha zinazojumuisha mchakato wote, ukianzia wakati wa kuundwa kwa Tume Maalum ya Mabadiliko ya Katiba na pia kuwapo kwa vikao vya Bunge Maalum la Katiba vilivyofanyika mjini Dodoma.



Hali ya usafi soko la Mabibo, maarufu kama Mahakama ya Ndizi, jijini Dar es Salaam ni mbaya kutokana na kukithiri kwa tope jingi na uchafu sokoni humo jana, kitendo kinachoweza kusababisha magonjwa ya mlipuko kikiwemo kipindupindu. **PICHA: SALOME KITOMARI**

# Matatani madai ya kukutwa na kobe 438

**Na Ndalike Sonda,** SIMIYU

JESHI la Polisi mkoani Simiyu linamshikilia mkazi wa Bunda, mkoani Mara kwa tuhuma za kukutwa na kobe 438 wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 71.16.

Akizungumza jana mjini Bariadi na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Richard Abwao, alisema mtuhumiwa huyo ambaye jina lake limehifadhiwa, alikamatwa Machi 2, mwaka huu, majira ya saa mbili usiku katika kata ya Dutwa, wilayani Bariadi.

Kamanda Abwao alisema kuwa kobe hao walikuwa wamehifadhiwa kwenye mabegi matatu aliyokuwa anasafiri nayo.

Alisema mtuhumiwa huyo kwa sasa yupo mahabusu na uchunguzi wa tukio hilo unaendelea kabla ya kumfikisha mahakamani. Kamanda Abwao alisema kuwa kobe hao wamekabidhiwa kwa maofisa maliasili kwa ajili ya hifadhi.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kujiepusha na umiliki wa nyara za serikali kinyume cha sheria kwa kuwa kufanya hivyo ni kosa la jinai. Kadhalika, aliwataka wananchi mkoani Simiyu kuendelea kutoa taarifa za wahalifu na uhalifu katika makazi yao ili kuufanya mkoa huo kuwa salama kwa kuishi.

# Serikali yasikia kilio makato ya mikopo wanafunzi elimu ya juu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SAKATA la makato makubwa kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu, limeibuliwa tena bungeni na wabunge huku serikali ikiahidi kufanya mapitio Sheria ya Bodi ya Mikopo kuangalia namna ya kupunguza au kuondoa riba na tozo zinazolalamikiwa.

Novemba mwaka 2016, Bunge lilipitisha marekebisho katika Sheria ya Bodi hiyo Sura ya 178 ambapo mnufaika wa mkopo anarejeshe mkopo kwa makato si chini ya asilimia 15 ya mshahara wake kila mwezi na kutoza asilimia sita kama tozo ya kutunza thamani.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, Mbunge wa Mbozi (CCM), George Mwenisongole, alihoji kwa nini serikali isipunguze riba kwa wanaolipa deni lote kwa mkupuo kwa wakati mmoja kutoka asilimia 10 ili iwe asilimia mbili au tatu za kupunguza tozo ya kutunza thamani ambayo ni kubwa na haipo kwenye mkataba wanaojaza wakati wa kukopa.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Halima Mdee alisema serikali imekuwa ikisema mikopo hiyo inawasaidia watoto wa familia maskini lakini mikopo hiyo imekuwa ni mzigo kwa watoto hao.

"Kuna makato ya mshahara asilimia 15 kila mwezi, kuna interest rate asilimia 10 kwa walioshindwa kulipa ndani ya miezi 24 kuna asilimia sita ya interest kwa watu wanaolipa badala ya kuwa ni mkopo wa kusaidia watoto unakuwa mkopo wa kibiashara, lini serikali italeta bungeni mabadiliko ya kisheria?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, alisema serikali itafanyia mapitio ya tozo pamoja na riba ili kuangalia namna ya kuzipunguza au kuziondoa ili kukidhi mahitaji kutokana na malalamiko yaliyopo.

"Tunaomba mtuachie jambo hili tukalifanyie kazi, muwe watulivu ili kuhakikisha mikopo hii haiwi kero kwa wananchi maskini,"alisema.

Akitoa majibu ya nyongeza, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema katika mapitio hayo wanafanyia kazi tozo ya asilimia sita ya kutunza thamani na hakuna riba ya asilimia 10.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Busokelo (CCM), Atupele Mwakibete, alisema kumekuwapo na tatizo kwenye mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu hususan kwa wanafunzi ambao hawana uwezo.

"Je, ni kwa kiwango gani serikali inajiridhisha kuwa inatoa mikopo kwa wanafunzi walengwa," alihoji.

Naibu Waziri Kipanga alisema serikali inajiridhisha kuwa inatoa mikopo kwa wanafunzi walengwa kupitia vigezo vilivyowekwa na sheria hiyo ambayo inawalenga wanafunzi wa kitanzania wenye sifa za kujiunga elimu ya juu lakini kutokana na hali ya kiuchumi hawana uwezo wa kumudu gharama.

"Ili kuwafikia wahitaji wengi zaidi, sheria imetoa mamlaka kwa bodi kuweka vigezo vya ziada ambapo katika mwaka wa masomo 2020/21, serikali kupitia Bodi ya Mikopo ilitangaza mwongozo wa utoaji mikopo uliotaja sifa na vigezo vya ziada ikiwemo yatima.

"Mwombaji au mzazi mwenye ulemavu, Mwombaji aliyefadhiliwa katika masomo yake ya sekondari au stashahada (diploma) na Mwombaji anayetoka kwenye familia ya kipato cha chini au kaya maskini," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa kuzingatia sifa na vigezo hivyo katika mwaka wa masomo 2020/21, jumla ya waombaji wapya 66,374 wenye sifa za kujiunga na elimu ya juu waliomba mkopo na kati yao waombaji 55,318 (83%) walipangiwa mkopo ambao ni yatima (1,137- 2.06% ), waliofiwa na mzazi mmoja (8, 683- 15.70% ).

"Waombaji wasiowafahamu wazazi au kulelewa katika Vituo vya Ustawi wa Jamii 71 sawa na asilimia 0.17, waombaji wenye ulemavu au wenye wazazi walemavu (92 ambao ni asilimia 0.13, waombaji waliofadhiliwa na taasisi zinazotambulika 1,992 asilimia 3.6 na Waombaji kutoka kaya masikini 43,343 sawa na asilimia 78.35," alisema.

# Wabuni mbinu mpya kuozesha wanafunzi

**Na Christina Haule,** KILOSA

WAZAZI katika wilaya ya Kilosa, wamedaiwa kuibua mbinu mpya ya kuozesha watoto wao wanaosoma shule za msingi na sekondari kwa kutumia vibali vya uhamisho kuwa wanawapeleka shule zingine ndani na nje ya wilaya na mkoa.

Kutokana na hali hiyo, walimu wakuu na wakuu wa shule za msingi na sekondari wametakiwa kuacha tabia hiyo, vinginevyo wataingizwa kwenye kesi za kuoza wanafunzi na kuwakatishia masomo.

Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Kilosa, Laurence Mlaponi, alisema hayo jana wakati wa kikao kilichoandaliwa taasisi isiyo ya kiserikali inayojishughulisha na utoaji wa elimu kwa jamii ya DIRA.

Kikao hicho kilikuwa na lengo la kukutana na wadau kujadili mafanikio ya mradi wa mpango wa kusimamia na kufuatilia rasilimali za umma (PETS) chini ya ufadhili wa The Foundation For Civil Society (FCS).

Mlaponi alisema walimu wakuu wanapaswa kuamka na kuacha mara moja vitendo vya kuwaamini wazazi na kutoa vibali vya uhamisho kwa wanafunzi bila kuhakikisha na kuthibitisha katika shule wanazokwenda kwa sababu wazazi wengine wamekuwa wakitumia nafasi hiyo kuwapeleka watoto wao kuolewa.

"Wapo wazazi wanaenda shule kuomba kuhamisha watoto wao mfano anasema anampeleka wilayani Makete, Njombe ambako ni mbali akiamini mwalimu hawezi kuuliza kumbe si kweli na sababu mwalimu ataona uvivu kuthibitisha hilo atatoa kibali. Hiyo itawagharimu nao walimu wataingia kwenye kesi ikibainika kuna udanganyifu," alisema.

Naye Diwani wa Tindiga, Yahaya Mbachi, alisema suala la wanafunzi kuacha shule na kuendelea na mambo yao mbalimbali ya kijamii linapaswa kuchukuliwa hatua kutokana na kuendelea kushika kasi katika maeneo mengi ya vijiji kwa sasa.

Alisema wako watoto ambao ripoti zao zinasomeka shuleni kuwa wamehamishwa au wamefariki dunia jambo ambalo si kweli na hali hiyo imetokea kwa sababu mwanafunzi ameolewa au amepata ujauzito.

Mbachi alisema walimu wanapaswa kuwa macho na suala hilo kwa kuwa wako wazazi ambao hulazimisha kuwatoa nje ya mfumo wa shule watoto wao ili wasiingie kwenye matatizo pale mtoto atakapoonekana kutofika shuleni kwa kipindi kirefu.

## Shule watoto wanayotembea kilometa 25 yapatiwa mabati

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA), imekabidhi msaada wa mabati kwa shule tano ikiwamo ambayo wanafunzi wake wamekuwa wakitembea kilometa 25 kila siku kwenda shuleni na kurudi nyumbani.

Msaada huo ulitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye, ambaye aliukabidhi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara na Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Geuzye alisema walipokea mabati 500 yenye thamani ya Sh. milioni 12 kutoka kampuni ya Yallin Global.

"Kwa kawaida TEA hupokea maombi ya uboreshaji na ujenzi wa miundombinu ya elimu ambayo hutoka katika halmashauri mbalimbali na huonyesha ukubwa uliopo, leo tumekabidhi mabati 500 kwa shule tano, ambapo mbili ni za Kigamboni na tatu za wilaya ya Babati," alisema.

Geuzwe alizitaja shule hizo kuwa ni Maleshi, Majengo na Kazarogo zilizoko Babati na Ugingoni na Raha Leo za Kigamboni.

Alisema kutokana na uhitaji wa uboreshaji wa miundombinu katika elimu ni mkubwa, amewaomba wadau kujitokeza kuchangia vifaa au fedha taslimu kupitia mamlaka hiyo.

"Baada ya elimu bila malipo kumekuwa na udahili mkubwa wa watoto wengi shule za msingi na wanakwenda kuongeza idadi kubwa shule za sekondari, mahitaji nayo yanakuwa makubwa siku hadi siku," alisema.

Geuzye aliwaeleza wadau wa elimu kuwa kuchangia miradi ya elimu kupitia TEA itawawezesha kutambulika kwa kupewa hati ya utambuzi ya uchangiaji elimu ambayo inamsaidia kupata nafuu ya kodi kwa kuomba kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, John Nchimbi, alisema wakati maeneo ya mjini wakilalamikia shida ya madawati, wao wanazungumzia matatizo ya wanafunzi kutembea kilometa 25 kila siku kwenda kutafuta elimu na kurudi nyumbani.

"Unakuta mtoto wa darasa la kwanza mwenye umri wa miaka mitano au sita anatembea kilometa hizo kila siku. Leo tumepata msaada wa mabati ambayo yatapelekwa Shule ya Msingi ya Maleshi, kata ya Kashi, ambayo ili kufika kutoka kijiji cha Maleshi hadi katika shule hii ni kilometa 25, hivyo tuna mtoto leo tumemwokoa na kumpa tumaini ili atembee hata nusu kilometa," alisema.

Aliwaomba wadau wengine waendelee kuchangia sekta ya elimu kupitia TEA ili misaada hiyo iweze kuwafikia wanafunzi wa shule zilizopo pembezoni ambazo wao hawawezi kuipeleka moja kwa moja.

Mkurugenzi huyo alisema wananchi wamekuwa wakijenga madarasa na wanapofika kwenye kuezeka hukwama, hivyo msaada huo utasaidia kuondoa tatizo hilo.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, Charles Lawiso, alisema wilayani humo kuna maeneo ambayo bado hayajaendelezwa na kuna makazi ya watu ambayo mtoto hulazimika kwenda mbali kutafuta elimu kutokana na hudumа kutokuwapo kwenye makazi yake.

"Elimu bure imehamasisha wazazi kupeleka watoto shuleni hivyo kuna idadi kubwa ya wanafunzi na shule kuelemewa na kuwa na upungufu wa madarasa, madawati na ofisi za walimu, msaada huu wa mabati 250 kwa shule mbili Udingoni na Raha Leo, itasaidia kupunguza upungufu wa madarasa," alisema.


AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
*benki kwa maendeleo yako*



**Dkt. PHILIP ISDOR MPANGO**
MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SALAMU ZA PONGEZI

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na wafanyakazi wa Akiba Commercial Bank wanaungana na Watanzania wote kumpongeza **Dkt. Philip Isdor Mpango** kwa kuapishwa kuwa Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .

**Hongera sana.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la heri Rais Samia, Makamu Dk. Mpango

**JANA** Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango ameapishwa kushika nafasi hiyo ikiwa ni utekelezaji wa Katiba inayomtaka rais kupeleka jina la mtu anayeona anafaa kuwa msaidizi wake ambalo baada ya kupitishwa na Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi, lilipigiwa kura na Bunge.

Hatua zote hizo zimekamilika na kiongozi huyo ameshaapishwa na sasa amekuwa Makamu wa Rais ambaye atakuwa na wajibu wa kumsaidia rais katika utekelezaji wa majukumu yake ya kikatiba kwa manufaa ya Watanzania.

Dk. Mpango anafahamika kwa uchapakazi kwa kuwa kila alikopita alidhihirisha hilo na kuacha alama, ikiwamo msimamo wake hasa kwenye makusanyo na matumizi ya fedha za umma, kwa kuwa taaluma yake ya uchumi inamwezesha kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Amekuwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa miaka mitano jambo linalompa uzoefu na uelewa wa kutosha wa kile nchi inataka na nini kifanyike katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Akihutubia Bunge la Novemba, mwaka jana, Dk. Mpango alieleza alichokiona wakati akifanya kampeni za uchaguzi katika Jimbo la Buhigwe, kuwa ni kiwango cha umaskini wa wananchi na kwamba ni lazima hatua zichukuliwe kuwanusuru.

Jana, Dk. Mpango alieleza historia yake iliyoonyesha ni mtoto wa wazazi wa kawaida aliyelelewa katika familia ya kawaida na kusoma katika shule za kawaida, maana yake anayajua maisha ya Watanzania na nini kinatakiwa kuwakwamua kutoka kwenye lindi la umaskini. Rais Samia pia historia ya maisha yake ina mengi ya kujifunza na anajua hali ya maisha ya watu wa chini kabisa, ndiyo maana alitueleza alitaka kuingia kwenye Baraza la Wawakilishi ili akasimamie hoja za msingi ikiwamo kuwabana mawaziri ambao hawana majibu sahihi ya kinachoendelea kwa wananchi wa kawaida.

Wote wametoka chini katika familia za kawaida, wamepita sekta binafsi na serikalini hivyo wanayajua mazingira na changamoto zilizopo katika kila eneo, sasa wameshika usukani wa kuliendesha gari la kuivusha Tanzania kufikia uchumi wa kati wa kipato cha juu, kutoka uchumi wa kati wa kipato cha chini.

Matarajio ni makubwa kama kuhakikisha sekta binafsi inaimarika na kuzalisha kwa kuwa kwenye uchumi ndiyo injini, ikiachwa nyuma na kufubaa maana yake asilimia kubwa ya ajira na mapato yatakosekana. Kuna umuhimu mkubwa kuhakikisha sekta binafsi inaimarika ili itoe ajira kwa wingi na kuchangia uchumi wa nchi, kwa kuwa ni ukweli kuwa serikali haiwezi kuajiri watu wote wenye sifa za kuajiriwa.

Matarajio mengine ni kuhakikisha mashirika yasiyo ya kiserikali yanatekeleza wajibu wake ipasavyo kwa kuwa yakiachwa yakafanyakazi, yataajiri wengi na kuchangia uchumi wa nchi kupitia misaada mbalimbali ya kutekeleza miradi inayotolewa na wafadhili.


Kwa kuwa wote wana uzoefu na wamepita sekta binafsi maana yake tunatarajia kuona mabadiliko makubwa ambayo yatatoa ahueni ya maisha kwa kuwa sasa sekta binafsi itaweza kuajiri watu wengi na kuzalisha kwa wingi.

Matarajio mengine ni kutekeleza ahadi zilizopo kwenye Ilani ya CCM ambazo nyingi ni kumwondolea kero mwananchi wa kawaida kwa kupunguza au kumaliza umaskini, mapambano dhidi ya rushwa na uonevu.

Aidha, tunatarajia kuona uwajibikaji wa watumishi serikalini, nidhamu na uwazi katika utekelezaji wa majukumu, kuondoa uonevu, dhuluma, chuki na madaraja ambayo hayataliacha taifa salama.

Matarajio mengine ni vyombo vya habari kufanya kazi zake za kuelimisha, kuburudisha na kukosoa ili kuisaidia serikali kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Beatrice Moses

## Muungwana Lazima Nilonge

# Rais Samia amejua kuwapa faraja yao Watanzania

**BADO** Watanzania wangali ndani ya siku 21 za maombolezo ya kifo cha Hayati Dk. John Magufuli Rais aliyepokea kijiti cha uongozi wa nchi kwenye awamu ya tano, aliyetutoka Machi 17, mwaka huu.

Ilipofika Machi 19, mwaka huu, Samia aliapishwa kuwa Rais kwa mujibu wa katiba ya nchi. Ni baada ya kuapishwa taratibu nyinginezo, ikiwamo maandalizi ya kuzikwa kwa Hayati Dk. Magufuli ziliendelea kufanyika, hadi mchakato kutimia, nyumbani kwao Chato, mkoa wa Geita.

Taratibu za kuaga mwili wake zilifanywa kwenye mikoa mitatu ambayo ni Dar es Salaam, Dodoma kisha Visiwani Zanzibar na baadaye Mwanza, katika maeneo yote hayo wananchi walijitokeza kwa wingi kuaga mwili wa kiongozi huyo kisha kuzikwa wilayani Chato Machi 26, mwaka huu.

Katika kipindi hiki vyombo vyote vya habari nchini vilishamiri na habari za kumbukumbu ya matukio ya Hayati Dk. John Magufuli, kuanzia kwenye magazeti, hadi kwenye vituo vya radio na luninga mbalimbali.

Kwenye vituo hivyo, vinasikika ama kuonekana nyimbo za maombolezo kutoka kwa vikundi vya wanamuziki, zikiwamo kwaya na bendi tofauti nchini na wasanii wa kujitegemea, pia kunarushwa kumbukumbu za matukio kadhaa yanayomwonyesha Hayati Dk. Magufuli alivyokuwa akifanya kwenye mikutano ama ziara zake za kikazi.

Pamoja na kuwa katika kipindi hicho kigumu Rais Samia, ameonyesha uimara wake katika kuongoza kwa kuchukua hatua za kusimamisha kazi wazito katika asasi za umma, baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ambazo pamoja na mambo mengine, ilionyesha TPA imeingiza hasara ya mabilioni ya shilingi.

**Hili nalo liliwafanya wananchi wengi kutabasamu licha ya kuwa na majonzi wakiamini kuwa kiongozi huyo kutokana na uwezo wake kwenye masuala ya uchumi, atamsaidia rais kuiwezesha Tanzania kupiga hatua nyingine zaidi kwenye maendeleo kiuchumi hatimaye kijamii pia.**

Ni hatua iliyopokewa kwa tabasamu, wananchi wengi wakiamini kwamba imechukuliwa kwa nia njema, ili hatua zaidi za kisheria zichukuliwe kwa manufaa na maendeleo ya nchi.

Wakati wananchi wakiendelea kufurahia uamuzi huo, Rais Samia alipeleka jina la Philip Mpango, aliyekuwa Waziri wa Fedha kuwa ndiye aliyempendekeza kuwa Makamu wa Rais.

Hili nalo liliwafanya wananchi wengi kutabasamu licha ya kuwa na majonzi wakiamini kuwa kiongozi huyo kutokana na uwezo wake kwenye masuala ya uchumi, atamsaidia rais kuiwezesha Tanzania kupiga hatua nyingine zaidi kwenye maendeleo kiuchumi hatimaye kijamii pia.

Jana katika hafla ya kumwaapisha Makamu wa Rais Dk. Mpango, baada ya hotuba yake, Rais Samia alitangaza mabadiliko kadhaa aliyoyafanya kwenye Baraza la Mawaziri, huku akiwasisitiza kuchapa kazi kwa bidii na uadilifu na kuwa atakayeshindwa ataachwa njiani.

Pia aliweka sawa angalizo kwamba, wanaanza upya na wajipange kuelekea njia ya kusaka ufanisi kikazi. Hivyo, basi jumuiko la matukio haya kuanzia kumchagua Dk. Mpango hadi mabadiliko ya Baraza, tukio la jana alasiri, yanaendelea kwa kuwashtukiza wananchi.

Hata hivyo, raha yake ni wazi pia yanaonekana kuwafurahisha wengi, hivyo kuthibitisha ule msemo wa wahenga kuwa 'baada ya dhiki ni faraja.'

HABARI KITAIFA

# Mifumo ya ununuzi wa umma yaunganishwa

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

SERIKALI imesema kwa sasa Mfumo wa Ununuzi wa Umma (TANePS) tayari umeunganishwa na Mfumo wa Kukusanya Mapato ya Serikali (GePG) na taratibu zinaendelea ili kuunganisha na mifumo mingine ya serikali ili kuongeza ufanisi.

Hayo yalisema jana jijini Dodoma na aliyekuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mwanaidi Ali Khamis, alipokuwa akijibu swali la Msingi la Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa.

Silaa aliuliza kama serikali haioni haja ya kurejesha mfumo wa TANePS Hazina ili ukatekelezwe na kusimamiwa pamoja na GePG katika kuongeza ufanisi.

Alisema kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 pamoja na kanuni zake, serikali inaendelea kuboresha utendaji wa Mfumo wa TANePS ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za ununuzi na haioni haja ya kuuhamishia mfumo huo Hazina kwa sasa.

"Kifungu cha 9 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma kimeipa nguvu Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), kuanzisha na kusimamia mifumo na taratibu zote zinazohusu masuala ya ununuzi wa umma ikiwa ni pamoja na mfumo wa TANePS," alisema.

Mfumo wa TANePS, alisema umetayarishwa kukidhi matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ambayo imeweka misingi na taratibu zinazohimiza uwazi, usawa na haki katika michakato ya ununuzi ili kuipatia serikali thamani halisi ya fedha zinazotumika katika ununuzi wa bidhaa na huduma mbalimbali.

Katika hatua nyingine, alisema wateja waliowekeza amana inayozidi Sh. milioni 1.5 katika Benki ya Wananchi Meru kabla ya kufungiwa kutoa huduma za kibenki mwaka 2018 watalipwa kiasi kilichobaki chini ya zoezi la ufilisi.

Alisema kwa mujibu wa sheria na taratibu za ufilisi, kiasi kitakacholipwa kitategemea fedha zitakazopatikana kutokana na kuuza mali za Benki husika ambapo zoezi la kukusanya madeni na mali za Benki ya Wananchi Meru linaendelea.

Khamis alisema hayo alipokuwa akijibu swali la Msingi la Mbunge wa Arumeru Mashariki aliyehoji ni lini serikali itatoa amana na hisa za wateja waliokuwa wamewekeza katika Benki ya Wananchi Meru kabla ya kufungiwa.

"Hadi kufikia mwishoni mwa Februari, 2021, jumla ya Sh. bilioni 1.47 zimeishalipwa kwa wateja waliokuwa na amana katika benki hiyo. Malipo hayo ni sawa na asilimia 78.70 ya Sh. bilioni 1.86 zilizotengwa kwa ajili ya kulipa fidia," alisema.

Pia alisema wateja waliolipwa ni 4,679 kati ya 13,138 ikiwa ni asilimia 35.61 ya wateja wote waliokuwa na amana zilizostahili fidia.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT), iliifutia leseni ya kufanya biashara ya kibenki Benki ya Wananchi Meru kwa mujibu wa Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006.

Aidha, iliiteua Bodi ya Bima ya Amana kuwa mfilisi ambapo ilianza zoezi la kulipa fidia ya Bima na Amana ya hadi Sh. milioni 1.5 na kazi hiyo inaendelea.

# Auawa pembeni wakutwa ujumbe 'mke wa mtu sumu'

**Na Rose Jacob,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za mauaji na wengine 20 akiwamo mwalimu wa Shule ya Msingi Kishiri jijini Mwanza kwa tuhuma za wizi wa vitabu zaidi ya 500.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Muliro Jumanne Muliro, alisema katika tukio la mauaji, watuhumiwa ambao majina yao yamehifadhiwa wanadaiwa kumuua, mwanaume anayekadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 40 hadi 42 kwa madai ya kutembea na mke wa mtu.

Kwa mujibu wa Kamanda Muliro, tukio hilo lilitokea juzi katika kata ya Mkuyuni, wilayani Nyamagana na kwamba pembeni mwa mwili wa marehemu kulikuwa maandishi yaliyoandikwa kwenye sakafu kuwa 'mke wa mtu ni sumu'.

Kamanda Muliro alisema watuhumiwa wote wanashikiliwa na jeshi hilo na baada ya upelelezi kukamilika watafikishwa mahakamani.

Alisema katika tukio lingine, mwalimu wa shule ya msingi, Mengi Mheta, anashikiliwa kwa kosa la kuuza vitabu vya wizi.

Alisema vitabu hivyo vinadaiwa kuibwa katika shule tatu tofauti za msingi wilayani Kwimba, mkoani Mwanza na kuuzwa na mwalimu huyo kwenye maduka ya wafanyabiashara.

Kamanda huyo alisema vitabu hivyo ambavyo ni vya serikali viliibwa katika shule za msingi za Bujengwa, Igoma na Manguluma, zote za wilayani Kwimba.

Alitaja vitabu hivyo kuwa ni vya Kiingereza na Kiswahili na kwamba wizi huo ulifanyika kwa ushirikiano wa walimu na walinzi wa shule hizo tatu.

Alisema baada ya kutokea wizi huo, watuhumiwa walitengeza njama za kufikirika kwamba kulitokea wizi na walinzi walifungwa kamba jambo ambalo wamebaini ni la uongo.

Alifafanua kwamba baada ya watuhumiwa hao kuiba vitabu hivyo walifuta nembo iliyowekwa yenye katazo la kutouza mali hiyo.



# Bil. 13/- zatengwa ukarabati barabara

**Neema Sawaka,** KAHAMA

WAKALA wa Barabara Nchini (TANROAD), Mkoa wa Shinyanga, umetenga Sh. bilioni 13.4 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za mkoa huo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Meneja wa TANROAD Mkoa wa Shinyanga, Mibara Ndilimbi, alisema kwamba wanahudumia mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometa 1004.59, kati ya hizo za changarawe ni kilometa 741, lami kilomita 251 na za udongo kilometa 753.52 kwa mkoa mzima.

Alisema, kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 TANROAD inatekeleza mikataba 44 na inatarajia kufikisha mikataba 50 kwa kutumia zilizotengwa mfuko wa barabara ili kutekeleza miradi ya matengenezo ya barabara, madaraja na makaravati ya Mkoa wa Shinyanga.

Alisema, licha ya jitihada zinazofanywa na TANROAD katika Mkoa wa Shinyanga za kuimarisha barabara, madaraja na makaravati wanakabiliwa na changamoto ya ucheleweshwaji wa misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT), kwa kuwa miradi yote ya serikali inatakiwa kutekelezwa bila ongezeko la kodi ya thamani.

Changamoto nyingine ni uhaba wa vifaa vya makandarasi kwa kuwa miradi yote huanza kwa wakati mmoja na kwa nchi nzima na wafanyakazi ni hao hao.

Baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Kishapu, mkoani Shinyanga, walishukru TANROAD kwa kujenga Daraja la Negezi katika Barabara ya Kanawa Mihama, ambalo litawasaidia kusafiri na kupita kwa usalama ikiwamo kusafirisha mazao yao na malighafi kwenda kwenye masoko.

# Waliofariki dunia ajali ya gari waongezeka

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

IDADI ya watu waliokufa katika ajali ya basi la Kampuni ya Machame Investment linalofanya safari zake, kati ya miji ya Dodoma, Arusha na Moshi, imefikia wanane.

Basi hilo lenye namba za usajili T 479 DRF, aina ya Youtong, lilipata ajali juzi alasiri katika eneo la mteremko wa kiongozi, Wilaya ya Babati mkoani Manyara na kusababisha majeruhi 53.

Akitoa taarifa jana kuhusu hali za majeruhi wa ajali hiyo, Kaimu Mganga Mkuu wa Mji wa Babati, Dk. Aretas Laurent, alisema vifo vilivyotokea mpaka sasa vinawahusu wanaume watatu na wanawake watano, kati yao mmoja alikuwa mtoto.

"Hadi kufikia jana kulikuwa na ongezeko la vifo viwili na kufanya idadi ya waliofariki kufikia wanane, badala ya sita. Tulipokea majeruhi 34 wanaume na wanawake 19," alisema. Alisema kati ya majeruhi hao, waliowapokea wanne hali zao ni mbaya na wamepewa rufani kwenda Hospitali ya Kibingwa ya Benjamin Mkapa, mkoani Dodoma, Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC na Hospitali Teule ya Misheni ya KKKT ya Seliani, Arusha.

Dk. Aretas, aliwataja waliofariki dunia katika ajali hiyo na kupokelewa katika Hospitali ya Babati kuwa ni dereva wa basi hilo, Seleman Lema na kondakta wake aliyefahamika kwa jina moja la Zacharia.

Wengine ni Ariana Koira, Quen Mollel, Petrolina Joseph, Leodguard Kalinge na Gloria Samu. Kwa mujibu wa Dk. Aretas, miili ambayo imeishatambuliwa mpaka sasa na kuchukuliwa na ndugu na jamaa zao ni miwili, ambayo mmoja ulichukuliwa saa 9:00 usiku na mwingine asubuhi ya Machi 31, mwaka huu.



Tope na uchafu vikiwa vimewazingira wafanyabiashara katika soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatarishi kwa afya zao na wateja wao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# WLAC yataka ufuatiliaji haki wafanyakazi wa sekta binafsi

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake na Watoto (WLAC), kimeziomba mamlaka zinazohusika na ukaguzi na ufuatiliaji wa haki za wafanyakazi katika sekta zote kuhakikisha zinafanyia kazi upungufu ili kuwasaidia kupata haki zao za msingi.

Akizungumza hivi karibuni wakati wa semina kwa viongozi wa serikali za mitaa katika Mkoa wa Dar es Salaam, Mwanasheria wa WLAC, Consolata Chikoti, alisema bado kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za wafanyakazi katika taasisi nyingi hasa sekta binafsi.

Alisema miongoni mwa haki za wafanyakazi zinazokiukwa ni pamoja na kunyimwa mikataba ya ajira, kufukuzwa kazi kiholela, kunyimwa likizo, kunyanyaswa kingono na kunyimwa malipo ya kazi za ziada.

"Ukiukwaji wa haki za wafanyakazi upo katika maeneo tofauti, kama wanasheria, tumekuwa tukifanya kazi ya kutembelea katika taasisi mbalimbali ikiwamo sekta rasmi na isiyo rasmi, tumebaini hakuna uzingatiaji wa muda wa kazi, likizo za uzazi, ukatili wa kingono, ugonjwa, usalama wa wafanyakazi na wengine wanaumia na hawalipwi fidia," alisema Chikoti.

"Wafanyakazi wengi hawapewi mikataba, wanafukuzwa bila sababu za msingi na bila kufuata taratibu za kisheria na ukiukwaji mkubwa upo sana katika sekta isiyo rasmi."

Alisema ipo haja kwa maofisa kazi kuhakikisha wanaongeza kasi ya kuwatembelea waajiri, kuwakagua na kusimamia utekelezaji wa haki za wafanyakazi.

"Tunaamini kwamba wamekuwa wakiwatembelea waajiri, lakini tunaomba waongeze kasi kuhakikisha wanawafikia wote na kushughulikia kero wanazozibaini kwa sababu hapo ndipo kwenye tatizo," alisema Chikoti.

Ofisa Mtendaji Kata ya Kinondoni, Flora Mazengo, alisema wanapokea malalamiko kutoka kwa wafanyakazi kunyimwa haki zao.

"Kwa upande wa Kinondoni tumekuwa tukipokea malalamiko kwa wafanyakazi kwamba waajiri wengi wamekuwa wakiwanyanyasa kwa kutokuwapa stahili zao, wengine hawapewi mikataba kabisa hasa kwenye viwanda na wanalazimika kufanya kazi hizo kwa sababu ya shida walizonazo," alisema Mazengo.

"Inabidi hawa waajiri hasa kwenye viwanda wawe wanakaguliwa mara kwa mara maana kuna maovu mengi yanajificha huko makazini, tunaamini kwa kuwatembelea na kuwakagua itasaidia na watakuwa wanafuata taratibu za kazi kama sheria zinavyoelekeza."

# Wananchi wavamia ofisi ya kata kutaka hatima viwanja vya wazi

**Na Romana Mallya**

WANANCHI wa Mikocheni A wamevamia ofisi ya kata ya eneo hilo kwa ajili ya kumtaka diwani wao awaeleze hatima ya viwanja vya wazi vilivyochukuliwa na watu binafsi na kusababisha wao kukosa huduma muhimu za kijamii.

Wakazi hao walifika jana asubuhi kwenye ofisi ya Ofisa Mtendaji wa Kata Mikocheni mkoani Dar es Salaam na kukutana na diwani wao, Mhandisi Hussein Zenzely.

Wakizungumza mbele ya diwani huyo, walisema wamelazimika kwenda hapo baada ya kuona maeneo ya wazi yaliyopo Mikocheni yameanza kujengwa na kutoa mfano eneo maarufu la Mabwawani ambalo lilisimama ujenzi baada ya kulalamika, lakini wiki moja iliyopita umeanza tena.

Magdalena Mkeka, alisema kukosekana kwa huduma za kijamii Mikocheni A kumesababisha wanapougua kutumia gharama kubwa kufika hospitali.

"Tuna maeneo ya wazi ambayo yametengwa, lakini cha kushangaza kwa sasa yanajengwa na watu binafsi na kusababisha wananchi kukosa hata zahanati, ukiugua unalazimika kukodi gari likupeleke Mwananyamala kwa Sh. 40,000, uwezo huu hatuna," alisema.

Alisema huduma nyingine ya kijamii ambazo hawana licha ya kuwa na maeneo ya wazi kuwa ni soko na viwanja vya michezo.

"Watoto wetu wakitaka kucheza wanavuka barabara ya Ali Hassan Mwinyi wakigongwa na magari, viwanja vipo mfano Mabwawani tulipewa, sasa kwa nini mtu amiliki kiwanja cha wananchi, tunamwomba Rais Samia Suluhu Hassan, atuone Mikocheni tunavyopata shida.

"Tunamwomba atusaidie viwanja hivi virudishwe ili ipatikane hospitali, viwanja vya michezo na soko na tuna tatizo la barabara mvua ikinyesha ni shida hazipitiki."

Alisema wameamua kwenda kwenye ofisi hizo ili kudai haki hizo pamoja na kero nyingine muhimu na kutaka ziwasilishwe ngazi za juu na kupatiwa ufumbuzi.

Said Hamad, alisema tangu Tanzania ipate uhuru Mikocheni haijawahi kuwa na zahanati wala sehemu ya michezo licha ya kuwapo maeneo ya wazi.

Akijibu malalamiko hayo, Diwani Zenzely alisema, Mikocheni A kuna tatizo la maeneo ya wazi kuvamiwa na watu binafsi.

"Mfano eneo la wazi la Mabwawani limeshafika mbali tulianza kulisikia kwenye kata yetu na lilishafika manispaa linafanyiwa kazi, lina viwanja 12 na kuna watu wamemilikishwa, ili kujua wamemiliki vipi, nani amewamilikisha, tunaomba wananchi wawe watulivu ili tuweze kufuatilia zaidi," alisema.

Zenzely aliahidi wananchi hao kuwa atamwagiza Mtendaji Kata afuatilie suala hilo ili kupata muafaka wake.

"Mikocheni maeneo mengi yamevamiwa, wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu zilizofanyika mwaka jana eneo la Mabwawani wananchi walibomoa ukuta uliokuwa ukijengwa, hivyo ujenzi ulisimama na Machi 19, mwaka huu, tulipata taarifa ujenzi unaendelea, tutawaita waliomilikishwa ili watueleze walilipata eneo kutoka kwa nani," alisisitiza.

Alitaja maeneo mengine ya wazi yaliyopo Mikocheni kuwa ni pamoja na nyuma ya Hospitali ya Kairuki lenye ukubwa wa mita za mraba 400, jirani na shule binafsi ya Feza mita za mraba 1,800 na lingine la Ali Hassan Mwinyi lenye ukubwa wa mita za mraba 200.

## Ndivyo wananchi Tunduru wanavyomkumbuka JPM

**Na Stevie Chindiye**, TUNDURU

WAKAZI wa Kata ya Matemanga wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, wamesema watamkumbuka aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli kwa kuwapelekea takribani shilingi milioni 400 ambazo zimetumika kutatua kero za upatikanaji wa huduma ya afya katika eneo hilo.

Katika taarifa hiyo, wananchi hao wamemwelezea Hayati Magufuli namna alivyosimama katika kata yao wakati akiwa katika ziara aliyoifanya Aprili 6, 2019 na kupokea kero mbalimbali, na kwamba maagizo yote aliyoyatoa yalitekelezwa kwa kiasi kikubwa na yaliyo bakia ni ukamilishaji wa shughuli ndogo. Akizungumza kwa niaba ya wananchi hao, Diwani wa Kata , Hamisi Kaesa, ambaye alipewa mamlaka ya kufungua kituo cha afya Matemanga kwa niaba yake, alisema kwa sasa kituo cha afya kina waganga wawili ambao mtaalamu wa dawa za usingizi na wauguzi wapo wa kutosha.

"Kitendo cha Rais kunipa dhamana ya kufungua kituo cha afya kwa niaba yake kilinifariji sana na kuona kwamba kumbe pia serikali inanitambua na kujali utendaji wangu, hivyo katika msiba huu mimi najiona kama mwanafamilia," alisema Diwani Kaesa.

Alisema pia Hayati Magufuli wakati akiwa katika kata yake wananchi walimweleza juu ya uwapo wa kero za kutokuwapo kwa maji, na kuwa serikali iliwapelekea Sh. milioni 203.

Alisema kero nyingine iliyoelezwa na wananchi wakati wa ziara hiyo, ili kuwa ni ukosefu wa huduma ya umeme ambapo kutokana na maelekezo ya Hayati Magufuli, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alipeleka shilingi milioni 183 ambazo zimeshatekeleza maelekezo kwa kupeleka umeme kwenye vijiji na baadhi ya vitongoji vya kata hiyo.




Ofisa Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Tigo Pesa, Angelica Pesha, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa uzinduzi wa ushirikiano kati ya VISA na Tigo Pesa, ambapo wateja wake sasa wanaweza kuhamisha fedha kutoka akaunti zao za benki kwenda kwenye Tigo Pesa. Kushoto ni Mkuu wa Huduma za Fedha na Malipo wa Tigo Pesa, Mshamma Mshamma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Deni la bil. 16/- latesa chama cha ushirika

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

CHAMA Kikuu cha Ushirika cha Shinyanga (SHIRECU) kinadaiwa na Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB), Sh. bilioni 15.959 ambazo kilikopa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za chama.

Hayo yalibainishwa juzi kwenye mkutano mkuu wa chama hicho kilichokuwa na ajenda mbalimbali kwa ajili ya kukiimarisha.

Mwenyekiti wa SHIRECU, Lenis Jishanga, akijibu swali aliloulizwa na wajumbe wa mkutano huo ili kujua deni ambalo bado wanadaiwa na TIB, alisema baada ya kupunguza kulipa Sh. milioni 10, deni lililosalia ni bilioni 15.959.

Naye Joseph Mihangwa ambaye alikuwa Meneja Mkuu wa chama hicho wakati wa deni hilo, alitolea ufafanuzi kuwa deni halisi lilikuwa Sh. bilioni saba lakini kutokana riba kuwa kubwa limefikia kiasi hicho.

Aidha alisema wakati Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alipofika mkoani Shinyanga mwaka 2017 kuzungumza na wadau wa Pamba, aliunda tume kuchunguza ukubwa wa deni hil, na kubainika lilitozwa kimakosa. "Baada ya Tume ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kubaini deni hilo lilikuwa kimakosa, ndipo benki ya TIB ikasema iko tayari kulifuta na wakati huo lilikuwa limefika Sh. bilioni 11. Sasa tunashaghaa kufika hadi Sh. bilioni 15 ina maana halikufutwa," alisema Mihangwa.

Dotto Joshua, akisoma taarifa ya chama hicho kwa niaba ya Mwenyekiti wa SHIRECU, alisema moja ya changamoto kubwa ambazo chama kinapitia ni deni hilo na kusababisha kushindwa kufanya shughuli zingine za kuibua miradi ya maendeleo, zaidi ya kuishia kulipa madeni.

Pia alisema mikakati ya chama hicho kwa mwaka wa fedha wa 2021/22 ni kuanzisha miradi ya maendeleo ambayo itakinusuru chama kufa ni kuanzisha mradi wa unenepeshaji ng'ombe, mashine za kukoboa mpunga na kuchonga vyuma. Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, akizungumza kwenye mkutano huo, alikitaka chama hicho kisimame imara na kumaliza matatizo yaliyopo ili kiendelee kuhudumia wakulima na kununua mazao yao kupitia vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) na kuinua uchumi wao.

## Sababu kusitisha mafunzo zatajwa

WIZARA ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imetaja sababu tatu zilizofanya kusitishwa mafunzo ya JKT kwa vijana wa kujitolea kwa 2020/21 ikiwamo kufanya kutathmini mafunzo yaliyotolewa.

Waziri Elias Kwandikwa alitaja sababu hizo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Wingwi (CCM), Issa Kombo Omar, aliyetaka kujua ni kwa nini JKT imewarudisha nyumbani vijana ambao walishafika kambini kwa ajili ya kuanza mafunzo.

Akijibu swali hilo, Waziri Kwandikwa alitaja sababu hizo kuwa ni kutoa nafasi kwa JKT kutathmini mafunzo yaliyofanyika na kuandaa utaratibu wa kuwa na mitaala bora ya mafunzo ya vijana itakayowawezesha vijana hao kujitegemea wanapomaliza mafunzo badala ya kutegemea kuajiriwa.

"JKT kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na JKT kufanya mawasiliano na taasisi zingine kama, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) na Baraza la Mitihani (NECTA) kuandaa utaratibu wa kuongeza muda wa mafunzo ya vijana wa mujibu wa sheria kuwa mwaka mmoja badala ya miezi mitatu ya sasa na kuchukua vijana wengi zaidi wanaomaliza kidato cha sita huku idadi ya vijana wa kujitolea ikipunguzwa," alisema.

Pia alisema kutoa fursa kwa JKT kukamilisha mpango wa kuwawezesha vijana kupata mitaji wanapohitimu mafunzo kwa kushirikisha taasisi nyingine ambazo ni Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

"Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Kazi na Vijana na TAMISEMI, utekelezaji wa mkakati huu unasimamiwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa," alisema.

Aidha, alisema JKT itaendelea kutoa elimu kwa umma na kwa vijana wanaojiunga na JKT kujitolea kuelewa kwamba lengo la mafunzo ni kuwawezesha kujitegemea baada ya mafunzo hayo badala ya kutegemea ajira.




Habari zote na Augusta Njoji

# Tanzania yachangamkia soko la soya China

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema serikali imeanza kuchangamkia soko la maharage ya soya China na tayari imepeleka tani 140 Machi, mwaka huu.

Pia imesema imewaruhusu wafanyabiashara kununua maharage hayo na kupeleka kwenye soko hilo.

Bashe aliyasema hayo bungeni jana alipoulizwa swali la nyongeza la Mbunge wa Kuteuliwa (CCM), Humphrey Polepole, aliyetaka kufahamu mkakati wa serikali wa kukidhi soko hilo.

"China inatumia zaidi ya Dola za Marekani bilioni 40 kwa mwaka kununua maharage ya soya kutoka nchi 12 duniani. Tanzania hivi karibuni tumesaini mkataba nao na kuwa nchi ya 12 kupata soko hilo, tunatakiwa kupeleka kwa mwaka tani 140,000 na sisi uzalishaji wetu ni tani 14,000 kwa mwaka. Serikali imejipangaje kutumia soko la China wakati uzalishaji wetu ni mdogo?" Alihoji.

Naibu Waziri Bashe alisema serikali imeshaipa kazi Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kuongeza uzalishaji wa mbegu pamoja na kuondoa ukiritimba kwenye kusajili wafanyabiashara.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, alitaka serikali kubadili utaratibu wa kukopesha wakulima matrekta kutokana na mfumo uliopo kwa kuwa unawasababishia hasara. Akijibu swali hilo, Bashe alisema mikopo ya pembejeo na zana za kilimo yakiwamo matrekta kwa wakulima hutolewa kupitia mifumo mbalimbali.

"Mojawapo ya mifumo hiyo ni kupitia sekta binafsi ambapo kampuni zinazofanya biashara ya pembejeo na zana za kilimo hutoa mikopo kwa wakulima mmoja mmoja au kupitia vikundi," alisema.

Pia alisema mfumo mwingine ni kupitia taasisi za serikali kama Mfuko wa Taifa wa Pembejeo na Benki ya Maendeleo ya Kilimo ambazo hutoa mikopo yenye riba na masharti nafuu kwa wakulima kulinganisha na kampuni binafsi.

"Pamoja na kuwapo kwa mifumo hiyo, baadhi ya wakulima hushindwa kupata mikopo ya pembejeo kutokana na riba kubwa na masharti mengine yanayotolewa na watoa huduma," alisema.

Pia kutokana na kero hizo, alisema serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeanza kuwatambua watoa huduma wote wanaotoa mikopo ya pembejeo za kilimo yakiwamo matrekta ili kujua aina ya huduma na mikopo inayotolewa kwa wakulima.

Alisema hatua hiyo itasaidia kutambua kero zilizopo na kuzipatia ufumbuzi ikiwamo kupunguza riba, kuweka utaratibu unamwezesha mkulima kurejesha mkopo kulingana na mapato ya mkulima kwa msimu wa kilimo.

"Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo pamoja na Benki ya Maendeleo ya Kilimo zinaendelea kutoa mikopo yenye riba na masharti nafuu kwa wakulima ambapo zinatoa mikopo ya zana za kilimo ikiwamo matrekta kwa mkulima mmoja mmoja, vikundi na vyama vya ushirika kwa riba ya asilimia sita hadi 10 kulingana na aina ya mkopo," alisema.

Alisema katika mwaka 2020/21 hadi Februari, mwaka huu, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo umetoa mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 959.5.

"Kati ya mikopo hiyo, mikopo ya matrekta makubwa 16 yenye thamani ya Sh. milioni 729.5 imetolewa, Benki ya Maendeleo ya Kilimo imetoa mikopo ya matrekta makubwa 62 yenye thamani ya Sh. bilioni 5.6," alisema.

Hata hivyo, alisema ili kuongeza matumizi ya zana bora za kilimo na kuongeza tija katika kilimo, serikali imepanga kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha vituo vya kutoa huduma za kukodisha zana za kilimo kwa lengo la kusogeza huduma ya upatikanaji wa zana za kilimo kwa wakulima na kupunguza matumizi ya jembe la mkono kutoa asilimia 53 za sasa hadi kufikia asilimia 10 ifikapo 2025.



Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa, akijadiliana jambo na Waziri wa Katiba na Sheria, Mwigulu Nchemba (kushoto), Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde (wa pili kushoto) na Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bil. 14/- kuongezwa elimu bure

BUNGE limeelezwa kuwa katika mwaka wa fedha ujao 2021/22, serikali itaongeza Sh. bilioni 13.96 kwenye bajeti ya utekelezaji wa mpango wa elimu msingi bila malipo.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mtwara Mjini (CCM), Hassan Mtenga.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali wa kuongeza ruzuku katika mpango wa utoaji wa elimu ya msingi na sekondari bure.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema kwa mwaka ujao serikali inaomba kutengewa Sh. bilioni 312.09 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo ambalo ni ongezeko la Sh. bilioni 13.96 ikilinganishwa na Sh. bilioni 298.13 zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2020/21. Kwa mujibu wa Silinde, serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo kwa kadri ya mahitaji na upatikanaji wa fedha.

Alibainisha kuwa kuanzia Desemba, 2015 hadi Februari, mwaka huu, serikali imetoa Sh. trilioni 1.26 kwa ajili ya elimu ya msingi bila malipo.

Awali, Naibu Waziri huyo alifafanua kuwa utekelezaji wa mpango huo nchini ulioanza Desemba, 2015 na fedha zinazotolewa kupitia zinahusisha fidia ya ada, shughuli za uendeshaji wa shule, fedha za chakula kwa shule za bweni na malipo ya posho za madaraka kwa wakuu wa shule na maofisa elimu kata.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Mtama (CCM), Nape Nnauye, alisema katika utekelezaji wa mpango huo kuna matatizo yamejitokeza ikiwamo vigezo vinavyotumika kupeleka fedha vinasumbua hasa kwa shule zenye wanafunzi wachache wakati mahitaji ya kiutawala yanafanana na shule zenye idadi kubwa ya wanafunzi.

"Je, serikali haioni umefika wakati wa kupitia upya vigezo hivi na kuona namna bora ya kupeleka fedha hasa eneo la utawala ili kutatua tatizo hili na je, serikali haioni wakati umefika wa kutoa elimu bure kwa kidato cha tano na sita," alihoji.

Silinde akijibu maswali hayo, alisema serikali itaendelea kutenga fedha kulingana na mahitaji na kwamba suala la kidato cha tano na sita serikali imelipokea na italifanyia kazi kwa kuwa ni suala la kisera.

ama
ALHAMISI APRILI 1 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

## NDIVYO KILIVYO KIINI CHA WATOTO VICHWA VIKUBWA, MGONGO WAZI




Ukurasa 14

## KITENDAWILI CHA DAWA MIFUGO KUTIBU CORONA

PARFAIT KOLELAS

# Mpinzani mkuu wa Rais Sassou Nguesso aliyefariki kwa corona siku kabla kura

**Na Christina Mwakangale**

JANA safu ya makala ilikuwa inayomuhusu Rais wa Congo Brazzaville, Sassou Nguesso, aliyeshinda uchaguzi wa hivi karibuni na anaingia katika uongozi kwa kipindi kingine cha miaka mitano, baada ya kutumikia miaka 36.

Leo ni mwendelezo wa simulizi za mpinzani wake mkuu, rais aliyepo madarakani sasa, waziri wa zamani, aliyelazwa hospitalini kwa ugonjwa wa Covid-19, ikiwa ni wiki ya kutolewa matokeo ya chaguzi.

Parfait Kolélas, mmoja wa wagombea wakuu wa urais katika nchi hiyo, alifariki dunia saa chache baada ya kukamilika kwa shughuli ya upigaji kura nchini humo, Machi 21, wastani wa wiki moja na nusu iliyopita ingawa,

Siku mbili kabla ya kutolewa matokeo ya uchaguzi, Kolélas alipambana kutetea kiti chake katika siku ya mwisho ya kampeni, huku akiwataka wananchi kujitokeza kupiga kura.

Mkurugenzi wa kampeni yake, alisema Kolélas aliaga dunia akiwa katika ndege ya matibabu iliyokuja Brazaville, kumchukua, kwenda Ufaransa kwa matibabu.

Mwanasiasa huyo aliyefariki katika umri wa miaka 61 alipogundulika na virusi vya corona siku ya mwisho ya uchaguzi huo inatajwa ulipita shwari, ingawaje inaelezwa uliendeshwa kwa shwari, ingawa wapigakura wachache walijitokeza kushiriki uchaguzi huo kulingana na waangalizi.



Marehemu Parfait Kolélas, katika harakati zake kisiasa. **PICHA: MTANDAO**

Marehemu Kolélas alikuwa mmoja wa wagombea sita wa upinzani waliokuwa wanawania kiti hicho, dhidi ya Rais Sassou Nguesso.

Siku moja kabla ya uchaguzi picha ya video ilichapishwa ikimwonyesha Kolélas akiwa mnyonge akiwahimiza wapigakura kujitokeza kushiriki zoezi la upigaji kura.

Kolélas alikosa hafla yake ya mwisho ya kampeni Ijumaa baada ya kusema siku moja mapema kwamba anahofia alikuwa na malaria. Alilazwa katika hospitali ya kibinafsi katika mji mkuu, Brazzaville na baadaye ilithibitishwa alikuwa na Covid-19.

Akiongea kutoka kitandani mwake hospitalini, Kolélas alisema: "Ndugu zangu wapendwa, nina shida. Ninapambana na kifo. Walakini, ninawauliza jitokezeni na kupiga kura kwa mabadiliko. Nisingepigania bure."

Mkuu wa timu ya serikali ya kupambana na Covid-19, Elira Dokekias, anasema hali ya Kolélas ilikuwa mbaya Jumamosi na kisha Jumapili akahamishiwa kwenye kitengo cha corona katika hospitali ya Chuo Kikuu Brazzaville na angepelekwa nje ya nchi kwa matibabu.

Baada ya kupiga kura katika mji mkuu, Sassou Nguesso alimtakia ahueni ya haraka mpinzani wake, Kolélas, ambaye katika uchaguzi uliopita wa mwaka wa 2016.

Sassou Nguesso, alimshinda Kolélas, akipata asilimia 60 ya kura ikilinganishwa na asilimia 15 za mpinzani wake aliyefariki.

**HARAKATI ZA Kolélas**

Kolélas, ambaye alikuwa waziri, Oktoba mwaka 2015, nyumba yake ilizingirwa pia wafuasi wake 30 na askari wa walinzi wa rais walimzuia mtu yeyote kumtembelea.

Balozi wa Ufaransa nchini Congo-Brazaville, ndiye pekee aliruhusiwa kumpelekea chakula akiwa kizuizi cha nyumbani. Kolélas, ana uraia wa Ufaransa, pia Congo.

**ALIKOTOKA**

Guy Brice Parfait Kolélas, ndio jina lake kamili, alizaliwa Agosti 6, mwaka 1959, alifariki Machi 22, mwaka huu akiugua Covid-19.

Kolélas ni mwanasiasa ambaye alimrithi baba yake aliyeitwa Bernard Kolélas, aliyefariki, ambaye alikuwa Rais wa Chama cha Congolese Movement for Democracy and Integral Development (MCDDI).

Chama hicho kilikuwa kati ya vyama vikuu vya kisiasa vya Congo-Brazzaville.

Alikuwa pia mtumishi wa umma akiwa Waziri wa Uvuvi kuanzia mwaka 2007 hadi 2009, pia akiwa Waziri wa Utumishi wa Umma mwaka 2009 hadi 2015.

Alianzisha chama kipya kilichoitwa Union of Humanist Democrats, mwaka 2017. Mama yake Kolélas aliitwa Jacqueline.

Kolélas ni msomi wa uchumi, aliyepata shahada yake kutoka Chuo Kikuu Brazzaville's Marien Ngouabi, mwaka 1983.

Baada ya hapo aliendelea na masomo yake nchini Ufaransa na kutunukiwa shahada ya pili ya uchumi nchini humo, katika Chuo Kikuu Besançon mwaka 1985.

Kadhalika alipata shahada ya Usafirishaji Kimataifa Chuo Kikuu cha Mulhouse International Institute of Transport mwaka 1987.

Pia, alipata shahada ya juu ya udaktari wa falsafa katika Uchumi wa Viwanda, hususan kwenye mipango ya kibiashara kutoka Chuo Kikuu cha Dijon, nchini Ufaransa, mwaka 1993.

- ***Kwa mujibu wa taarifa mbalimbali.***

AFYA

BIDHAA YA TANGU 1918...

# Utupaji ovyo barakoa zilizotumika unavyohatarisha watoto, mazingira

## • Aina na matumizi, 'vigezo na masharti'



Wasafiri wakiwa wamevaa barakoa. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Dk. Raymond Mgeni**

DUNIA bado ipo katika mapambano dhidi ya mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona, maarufu Uviko. Ni mlipuko wa ugonjwa unaoendelea kuwapo kutoka mwishoni mwa mwezi Desemba wa mwaka 2019, pale iliporipotiwa mkasa wa kwanza nchini China.

Juhudi mbalimbali zinaendelea katika kudhibiti maambukizi, matibabu na utengenezaji wa chanjo ya Covid-19, huku chanjo zilizogunduliwa kuwa bado kunaendelea kuleta sintofahamu nyingi.

Moja ya juhudi hizo za udhibiti ziliainishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na nchini chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ni kufanya matendo kama unawaji wa mikono wa maji tiririka.

Mengine ni kujihami na utumiaji vitakasa mikono, uvaaji barakoa, kuepuka misongamano isiyo ya lazima, ufanyaji wa mazoezi kila siku na ulaji wa vyakula kujenga kinga ya mwili.

Juhudi za kudhibiti maambukizi ya Virusi vya Korona zimepokelewa kwa uzito duniani kote toka ulipotangazwa na WHO mwaka 2020.

### MZIZI WA BARAKOA

Ni mlipuko huo ulioanza na wimbi la kwanza na sasa limetokea wimbi la pili. Uvaaji barakoa au neno barakoa ndio lilipopata umaarufu mkubwa, janga la sasa lilipotokeza.

Licha ya uvaaji wa barakoa ulianza mwaka 1918 hadi 1919, ambapo mlipuko mwingine mkubwa wa mafua ya Kihispania uliotokea na kufanana na mlipuko wa sasa wa Covid-19, ambao uvaaji barakoa ulihimizwa sana.

Nchini Marekani mwaka 1918, paliwekwa sheria kabisa kuwa watu ambao walikataa uvaaji barakoa, basi walinyimwa kupata huduma za kijamii kama usafiri wa umma.

Sheria zilikuwa kali mno, hata kuzuia mikusanyiko katika umma, nyumba za ibada zilifungwa, sehemu za starehe nazo zilisitishwa kuepusha kuwa njia ya kusambaza maambukizi.

Dunia ikiwa katika jitihada mbalimbali za mapambano ya mlipuko wa Covid 19. Bado msisitizo wa uvaaji wa barakoa umeendelea kuwapo na kuzidishwa na kampeni kubwa inaendelea kufanyika maeneo mengi duniani, iliwekwa njia za mitandao au maeneo ya wakazi kwa maana ya matangazo au mabango.




Uvaaji barakoa umeoneka na hata kwa watu kuvaa wakiwa katika maeneo ya mikusanyiko ya watu kama shughuli za misiba, maeneo ya hospitali, nyumba za ibada, mikutano na nchini.

Wengi wamepata mwamko na wanatumia barakoa na wengine hawatumii, wanaotumia hususani ni barakoa maarufu ziitwazo 'surgical mask' au barakoa za upasuaji zinazokuwa zinatumika na madaktari wa upasuaji katika vyumba vya upasuaji kupendekezwa kuwa zinaweza kutumiwa na watu nje na maeneo ya hospitali.

Licha uvaaji barakoa kuhimizwa bado kumekuwa na mambo machache yasiyozingatiwa na watumiaji au uwezekano wachanga moto inazoweza kujitokeza baadaye.

Matumizi ya barakoa yanatajwa kuwa muhimu sana, maana inazuia maambukizi kwa asimilia kubwa, pale ambao watu wote huvaa.

Kama ilivyokuwa virusi vya corona vimekuwa vinasambaa, kupitia mfumo wa majimaji katika hewa ni rahisi kuepusha maambukizi hayo, ikiwa mtu atakuwa amevaa barakoa.

### BARAKOA INATENGENEZWAJE?

Utengenezaji barakoa upo katika namna nyingi. Zipo zinazotengenezwa na vyombo maalumu vilivyopata nafasi ya kutengeneza kama nchini, ni Bohari Kuu ya Dawa, ambayo barakoa za upasuaji 'surgical mask' zinazalishwa.

Aidha, zipo barakoa za muundo mwingine maarufu kama 'N95' na 'N99', zikiwa na maana hizo nambari '95' na '99' ni namna ilivyo na ufanisi mkubwa wa kuzuia vimelea vya magonjwa kutopenya na kuleta shida kwa mtu.

Pia zipo barakoa zinazotengenezwa kwa kutumia vitambaa na watu wameleta ubunifu mbalimbali wanatumia hata vitenge. Yote hiyo ni mapambano ya kuhakikisha kiwango cha maambukizi kinapungua kila siku, katika sehemu na mazingira tofauti.

Licha ya yote kumekuwa na uzagaaji au utupaji ovyo wa barakoa zilizokwisha kutumika hususani 'surgical masks' zinazotumika na mtu mmoja na si zaidi ya saa nne, inabidi kubadilishwa na kutupwa mbali.

Barakoa hizo zina rangi ya bluu bahari au bluu mpauko, ambazo mtu akiwa anapita maeneo ya miji, mifereji au penye zinakutwa sasa zimezagaa, hali ambayo ni hatari kwa kukaribisha maradhi ya corona.

### HATARI YA WATOTO

Ifahamike pia, watoto wana nafasi ya kusambaza virusi vya corona, hasa kwa siku moja na mbili tangu kupata maambukizi.

Wao wanaweza kuzichukua hizi barakoa na kuzitumia katika michezo yao ya utoto, pasipo kujua hatari iliyo mbele yao, pia kuchangia uchafuzi wa mazingira katika maeneo.

Utupaji wake unahitaji kuzingatiwa, huku katika baadhi ya maeneo kama ya hospitali, wana mifuko maalumu, pia dumu za taka zinazobeba barakoa zilizokwishatumiwa.

Ni vyema mtu anapomaliza kutumia atupe katika madumu ya taka mifuko ya taka, ili kuepusha uzagaaji holela na unaoweza kuleta madhara baada ya utupaji.

Mtazamo mwingine upo katika jicho la namna watu wanavyovaa barakoa hizi. Wapo ambao wanapokuwa wanakula au kutembea huzishusha hadi eneo la kidevu na kuzuivaa tena baadaye jambo ambalo kiafya haishauriwi, kwa maana kunaweza kupunguza ufanisi wa barakoa katika matumizi.

Hivyo, kanuni sahihi ni kuivaa barakoa, ila baada ya matumizi isitupwe ovyo katika mazingira, ili kuepusha kutumiwa na watoto, uchafuzi wa mazingira na hatari ya kuongeza uwezekano wa maambukizi ya virusi hivi.

***• Mwandishi anapatikana kwa mawasiliano: +255 676 559 211 na barua pepe: raymondpoet@yahoo.com***

AFYA

# NDIVYO KILIVYO KIINI CHA WATOTO VICHWA VIKUBWA, MGONGO WAZI

Na Sabato Kasika

WATOTO kuzaliwa wakiwa na vichwa vikubwa au mgongo wazi, ni miongoni mwa hali inayoendelea kujitokeza katika jamii, huku kasi ya kukabiliana nayo kiwango chake hakiridhishi sana, kwamba ushindi si wa kutosha katika kupambana nao.

Ni hali inayotajwa kuchangiwa na sababu ambazo madaktari na wadau wanaeleza, baadhi zipo ndani ya uwezo wa jamii, lakini kikwazo kikuu ni ukosefu wa elimu ya kutosha.

Wiki iliyopita, wadau walikutana kujadili kwa kina. Mustakabali huo na hatima yake chanya. Hapo panawajumuisha, pia Chama cha Wazazi wa Watoto wenye Ulemavu wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi Tanzania (ASBAHT).

Wengine katika mjumuiko huo wa kuzindua mafunzo ya kuvijengea uwezo vyombo vya habari, ni asasi za Child Help Tanzania na Chama cha Wazazi wa Watu Wenye Ulemavu wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi Zanzibar.

Mtazamo mkubwa ulikuwa kuvihamasisha vyombo hivyo na watendaji wake, kujikita katika masuala muhimu kijamii na kiuchumi, hasa lishe bora, huku wakikabili utapiamlo na udumavu.

Hapo ililenga kupunguza, kama sio kuondoa tatizo la uzazi wa watoto wenye ulemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi, kwa kuielimisha jamii kutambua athari za kukosa viinilishe muhimu, hasa 'foliki asidi'

Kwani foliki asidi ni nini? Ni aina ya Vitamini B inayoitwa 'folate' inayotengenezwa maabara na inafanya kazi muhimu ya utengenezaji chembe damu nyekundu inayosaidia utupu wenye taarifa za kiumbe (neural tube), katika kukua ubongo na uti wa mgongo.

Ni viini lishe vinavyopatikana zaidi kwenye, mboga zenye rangi kijani iliyokolea na matunda jamii ya chungwa.

Ni lini uanze kutumia asidi ya foliki? Inaalezwa, matatizo ya kuzaliwa mtoto huanza kutokea ndani ya wiki tatu hadi nne ya ujauzito.

Hivyo, ni muhimu kwa mjamzito kuwa tayari na 'folate' tayari kwenye mzunguko wa mwili katika kipindi hicho muhimu cha mwanzoni, ambao ndio ubongo na uti wa mgongo wa mtoto unajijenga.

**SABABU ZLIVYO**

Ofisa Mawasiliano wa Child Help Tanzania ambaye ni Katibu wa ASBAHT mkoa wa Dar es Salaam, Milton Byemerwa, anasema kuna walakini wa jamii, kuhusu uelewa wa kutosha kuhusu chanzo cha ugonjwa huo.



Mtaalamu bingwa, Dk. Consolata Shayo akielimisha kuhusu matumizi ya dawa na vyakula vyenye foliki asidi.

"Tumegundua kuwa jamii haina uelewa wa kutosha kuhusu chanzo, dalili, kinga na tiba ya tatizo hili. Wapo watu wanaopotosha kuwa ni ushirikina. Hili halina ukweli wowote, bali ni tatizo la kisayansi linalohusu lishe duni na njaa iliofichika," anasema.

Byemerwa anaongeza kwamba, kukosa taarifa muhimu kuhusu ulemavu kwa walio wengi ni miongoni mwa sababu zinazochangia kuendelea kuwapo watoto wanaozaliwa wakiwa na upungufu huo.

"Si ajabu hata miongoni mwetu hapa wapo wasio na uelewa wa kutosha juu ya jambo hili. Hivyo, hii ni fursa muhimu kwetu sote kuitumia kufahamishana masuala yahusuyo ulemavu huu, chanzo, dalili na tiba," anasema, akisisitiza hitaji la elimu ya kutosha kwa jamii kuelewa chanzo cha tatizo.

"Ikumbukwe kuwa, mtoto akishazaliwa akiwa na tatizo hilo, huwa ni la maisha yake yote na watu wanaohangaika ni kinamama, hivyo tusaidiane kutoa elimu ili jamii ibadilike," anasema.

Byeberwa anasisitiza umuhimu wa kupata elimu ya wataalamu kutoka maeneo kama Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI) na uzoefu wa wazazi na walezi wanaoishi na kulea wenye ulemavu wa aina hiyo.

Hapo anatoa msisitizo kwa taasisi zinazosaidia kuratibu masuala ya lishe, tiba, malezi na makuzi ya watoto hao.

**WAZAZI WAO**

Ramla Makame Juma kutoka Chama cha Wazazi wa Watu Wenye Ulemavu wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi Zanzibar, ana maelezo:

"Mimi nina mtoto wa aina hiyo, lakini, bahati nzuri familia ya mume wangu na ndugu zangu wapo pamoja nami, lakini kuna wanawake wengine wenye watoto wa aina hiyo wamekimbiwa na waume zao."



Ofisa Mawasiliano wa Taasisi ya Child Help Tanzania na Katibu wa ASBAHT Mkoa wa Dar es Salaam, Milton Byemerwa, akitoa mafunzo kwa washiriki. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

Kwanini hivyo? Ramla anataja sababu, kwamba ni ukosefu wa elimu ya kutosha kuhusu chanzo cha ugonjwa huo na kuna haja ya kupanua elimu zaidi, iwe na uelewa wa kutosha.

Fatuma Ally, kutoka Asasi ya ASBAHT Dar es Salaam, ana simulizi kwamba alikimbiwa na mume, baada ya kujifungua mtoto wa aina hiyo, lakini akajipa moyo na anaendelea kumlea mtoto kama kawaida.

**UNAJIKINGAJE?**

Consolata Shayo, ni daktari wa upasuaji wa wagonjwa vichwa vikubwa na mgongo wazi katika Hospitali ya MOI, mwenye nadharia ya namna ya kujihami kupata watoto wenye maradhi hayo.

"Anayetaka kuzaa, ni lazima ameze vidonge vyenye foliki asidi miezi mitatu hadi sita, kabla ya kubeba ujauzito na ni kidonge kimoja kila siku, pia kuzingatia lishe bora kwa kula vyakula vinavyotakiwa," anasema Dk. Shayo.

Anataja vyakula hivyo, ni mboga za majani zikiwamo kabichi, kisamvu, choroko, kunde, maharage, nyama, maziwa na mayai na nyingi zina bei ndogo.

Pia anatahadharisha kinamama kuacha kupendelea kula mlo wa chipsi kuku na chipsi mayai, akidai havina umuhimu kwa afya ya mtoto tumboni.

"Pia wanawake msikwepe kunywa vidonge vyenye foliki asidi, kwani baadhi yenu huwa mnadai kwamba vina harufu mbaya. Hivyo, msinywe pombe, kuvuta sigara au kuzaa katika umri mkubwa," anasema.

**VYAKULA VIRUTUBISHI**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, anasema, kuna mkakati wa kiserikali ulioko mbioni kutengeneza mashine nchini za kuongeza virutubishi katika unga zitakazotumiwa na wasindikaji wadogo na wakati.

Kwa mujibu wa Jenista, ni mkakati unaoandaliwa kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), pia Tume ya Sayansi an Teknoloijia nchini (COSTECH), pamoja na wadau wengine.

Meneja Mradi wa Programu za Uongezaji Virutubishi katika vyakula kutoka taasisi ya kimataifa ya Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN), Archard Ngemela, anaeleza umuhimu wa virutubishi lishe katika vyakula.

"Hayo yote ikiwamo utapiamlo yanatokana na upungufu wa virutubishi mbalimbali. Hivyo, ni muhimu kula vyakula vyenye virutubishi, yakiwamo mafuta ya kula, unga mahindi vingine," anasema.

Ngemela anataja hali zinavyoona, kwamba chakula cha binadamu, ndicho kinachobeba virutubishi mwilini kuupatia nguvu, kuusaidia kukua, hata kupambana na maradhi.

AFYA

# KITENDAWILI CHA DAWA MIFUGO KUTIBU CORONA

- Madaktari wapigia upatu, mamlaka hazitaki
- WHO yasita kwa kigugumizi...'inawezekana'
- Soko haramu limetawala bei iko juu mara 15

**Johannesburg, AFRIKA KUSINI**

VITA dhidi ya kuenea kwa corona duniani inachukua sura mbalimbali. Nchini Afrika Kusini, pia kuna hali kama hiyo, kila watu wakitafuta majibu kwa namna yao, baadhi yasiyo rasmi.

Kuna dawa aina ya Ivermectin, imekuwa ikitumiwa kutibu virusi vya corona huko Amerika Kusini, lakini bado haijathibitishwa kwa matibabu.

Hadi sasa dawa hizo za vidonge hazijaidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya binadamu na Mamlaka ya Udhibiti wa Viwango ya Afya (SAHPRA), bali imesajiliwa kama tiba ya minyoo ya wanyama.

Dawa ya Ivermectin imewagusa wengi nchini Afrika Kusini, ikihesabiwa kuwa dawa yenye ufanisi kwa tiba ya virusi vya corona, ingawa haijaidhinishwa kimatibabu.

Pamoja na kuwapo tafsiri hiyo ya kitaalamu, bado katika sura ya pili ambayo imekuwa tawala, ni dawa ambayo inadumu kuwa kiiovu cha makabiliano ya nchini Afrika Kusini.

Ndiyo aina ya sauti kutoka kwa baadhi ya madaktari wanaotaka ihalalishwe kisheria kuwa tiba kwa binadamu.

Hali iliyoko nchini Afrika Kusini inaelezwa si njema sana hivi sasa, kwani kuna raia wengi wanahangaika kusaka nyenzo ya kiafya inayoweza kupunguza athari za wimbi la tatu la maambukizi ya virusi vya corona.

Ilhali kuna mpango wa utoaji chanjo ambao haujawafikia wengi katika nchi hiyo iliyoathriwa zaidi na corona barani Afrika, kunatajwa kuwapo kundi lililoko kwenye hatari ya kuambukizwa zaidi msimu wa baridi utakapoingia.

Hadi sasa zaidi ya watu 52,000 wameshakufa kutokana na corona, ingawa maambukizi mapya kwa sasa yanakadiriwa yako chini.

Ni katika muktadha huu ambao - dawa inayotumiwa kuua minyoo - imepata imepata umaarufu na baadhi ya madaktari wamekuwa wakiitoa dawa kwa wagonjwa wenye virusi vya corona, wakidai wana ushuhuda inavyokabili athari mbaya za Covid-19.

Hata hivyo, wadhibiti viwango, watengenezaji wa dawa na baadhi ya wanasayansi wa juu nchini humo, wanatahadharisha matumizi ya dawa hiyo ya minyoo katika kutibu virusi vya corona.




Baadhi ya raia wa Afrika Kusini, wakidai mamlaka ziruhusu dawa ya Ivermectin itumiwe rasmi kutibu corona. Picha nyingine ni ya dawa hiyo. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**YAPATA UMAARUFU**

Raia nao wamekuwa wakidai kwamba, mamlaka zinaaswa kuruhusu dawa hiyo ya Ivermectin itumiwe na katika uhalisia mitaani, sasa imekuwa maarufu ikitawala masoko haramu nchini humo.

Ushahidi unadaiwa ni mamilioni ya tembe yanakamatwa nchini Afrika Kusini tangu mwanzoni mwa mwaka huu, huku upande mwingine, mitandao haramu ya uuzaji dawa hizo ikiendelea kuongezeka katika mataifa kama China na India.

Wakati awali dawa hizo haijahusishwa na virusi vya corona, tembe 10 ziliuzwa kwa bei wastani wa Dola za Marekani Nne (Sh. 9,200), sasa imeaanda mara 15 katika soko hilo hilo.

Baadhi ya madaktari, walianza kutumia dawa hizo, pindi Afrika Kusini ilipokuwa na viwango vya juu zaidi vya maambukizi ya corona mwezi Julai mwaka jana.

WAKATI WA KUTUKIA

Profesa Nathi Mdladla, Mkuu wa Kituo cha Tiba ya Dharura, katika Hospitali ya Chuo cha George Mukhari Academic, anasema madaktari wamashauri kutumiwa dawa hizo aina ya Ivermectin, pale kuna hali mbaya ya corona.

"Wakati maambukizi yalipokuwa ya juu zaidi katika wimbi la kwanza, hospitali zote za umma na za binafsi pamoja na madaktari wa kibinafsi nchini Afrika Kusini walikuwa wakitumia dawa ya Ivermectin," anatamka Profesa Mdladla.

Dakari huyo anaendelea: "Watu walikuwa wakifa na madaktari walikuwa wanaangalia aina mbalimbali za tiba, kujaribu kunusuru maisha ya watu. Ivermectin ilikuwa ni moja ya dawa ambayo ilitumiwa na madaktari ."

Anasema, waliupata mtazamo huo kutoka nchi za Amerika ya Kusini, ambako madaktari walitumia dawa hiyo. Hivi karibuni, baadhi ya tafiti zilionyesha kwamba zinaweza kuwa ya ufanisi, lakini kunahitajika ufuatiliaji zaidi.

Profesa Mdladla anasema uamuzi wao wa kutumia dawa hiyo isiyo rasmi kukabili corona, kwa kiasi kikubwa ilitumika hadi mwishoni mwa mwaka jana, ndipo wakaanza kuzuia matumizi yake, wakiwalazimisha madaktari kuacha kuitoa kwa wagonjwa.

Inaelezwa kwamba mamlaka ya kiserikali zinahofia kudhibitiwa kimataifa, pale itakapotumia dawa zisidhoidhinishwa. Hata hivyo, daktari huyo bingwa ana mtazamo wake kwamba, huo ndio msaada kwa familia zilizo masikini, ambazo hazimudu tiba ghali.

**CHANJO ILIPOANZIA**

Afrika Kusini ilianza mpango wa chanjo kwa umma mwezi Februari mwaka huu, huku kukiwapo sura inayokinzana.

Upande mmoja wa mjadala ni wahusika wa Mamlaka ya Udhibiti wa Viwango vya Afya hawaridhii dawa hiyo kutumika, huku upande wa pili vikundi vya utetezi na baadhi ya madaktari wanaitaka Ivermectin.

Ubishani huo hivi sasa uko katika mchakato wa kisheria katika Mahakama Kuu ya Gauteng. Hapo, daktari huyo wa binadamu, Profesa Mdladla akisema: "Mapambano ni juu ya ubora wa masomo ambayo yamefanywa hadi sasa.

Tunachosema ni kwamba, katika janga hilo, huwezi kamwe kuwa katika nafasi ya kutoa masomo haya ya kiwango cha juu na marefu, kwa sababu inamaanisha katika wakati huo huo, unaangalia watu wakifa."

Madaktari wanaotetea kuruhusiwa matibabu hayo kwa ugonjwa wa corona, wanasema dawa hiyo haina tishio lolote kwa usalama.

Mamlaka ya Kusimamia Chakula na Dawa ya Marekani, inataja ishara hadi ilizo nazo ni kama kujihisi kizunguzungu, kichefuchefu, kuhara, maumivu tumbo na upele wa ngozi.

**WHO NA INAVYOTIBIWA**

Dawa hizo zilishapendekezwa na Shirika la Afya Dunaini (WHO), katika nafasi yake kutibu aina fulani ya upofu, huku ikibainisha shaka kwamba hakuna utafiti wa kutosha kuhusu usalama wake.

Mnamo Desemba mwaka jana, WHO ilizuia utumiaji wa dawa hiyo kwa watu, isipokuwa madaktari na ikatoa idhini kupitia maalum iitwayo 'matumizi ya huruma' katika hali mbaya au mazingira magumu, katika sharti daktari atoea taarifa kuhusu maendeleo ya mgonjwa.

Namna gani inatibu? Nadharia mojawapo ni kwamba inawafaa walio na virusi vya corona, kutokana na uwezo wa kutibu vimelea vya aina yoyote na kuwafanya kuwa na nguvu.

Lakini, Mdhibiti wa Dawa Afrika Kusini kutoka SAHPRA, ana hoja kwamba: "Hakuna ushahidi wa kutosha kuhusu au dhidi ya matumizi ya Ivermectin katika kuzuia au kutibu Covid-19."

SAHPRA, pia inaelezea wasiwasi wake katika utumiaji dawa hiyo ya Ivermectin ipatikanayo zaidi katika soko haramu, akisema "ubora hauwezi kuhakikiwa."

Kampuni inayotengeneza dawa hiyo, Merck, inaonya utumiaji wake kwamba: "Hatuamini kwamba data (takwimu) inayopatikana inasaidia usalama na ufanisi wa Ivermectin, zaidi ya kipimo na idadi ya watu iliyoonyeshwa katika wakala wa kisheria aliyeidhinishwa kuagiza habari. "

Profesa Abdool Karim, mmoja wa madaktari anayeongoza ufuatiliaji majibu ya virusi vya corona ya Afrika Kusini, pia ameangazia dozi wanazopewa watu zina hatari hata ya kuwa sumu.

"Lazima isemwe wazi kwamba Ivermectin haiui virusi kwa kipimo ambacho binadamu anaweza kuvumilia. Kiasi cha dawa inayohitajika kuua virusi ni sumu kwa wanadamu. Chochote kinachofanya, sio kuua virusi," tovuti ya TimesLive inamnukuu mtaalamu huyo mtafiti wa corona.

- ***Makala hii ni kwa mujibu wa BBC.***



# Uvuvi bahari kuu kuboreshwa kwa kujenga bandari ya uvuvi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema kuwa katika bajeti ya sekta ya uvuvi ya mwaka 2021/22 imepanga kuboresha shughuli za uvuvi wa bahari kuu nchini na inatarajia kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi itakayo saidia kuongeza mapato yatakonayo na mazao hayo.

Katika bajeti hiyo Sh. bilioni 50 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo.

Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia sekta ya uvuvi, Dk. Rashid Tamatama, aliyasema hayo juzi wakati alipokuwa akiwasilisha bajeti ya wizara hiyo mbele ya Kamati ya Bunge ya Mifugo, Maji na Kilimo.

Alisema, katika bajeti hiyo maeneo ya vipaumbele ni pamoja na ujenzi wa bandari ya uvuvi itakayojengwa ili kuongeza ufanisi katika sekta hiyo nchini.

Dk. Tamatama, alisema kuwa hivi sasa mchakato wa kujenga bandari hiyo ya uvuvi upo katika hatua za kiuandaaji wa michoro na baada ya kukamilika hatua nyingine itafuata.

"Ili kuboresha shughuli hizi za uvuvi kuwa na tija na kuongeza pato la taifa kupitia sekta hii lazima tujenge bandari ya uvuvi itakayosaidia kuongeza uvunaji wa samaki tofauti na ilivyosasa na katika bajeti yetu hii tumetenga Sh. bilioni 50, kwa ajili ya ujenzi huo," alisema Dk. Tamatama.

Pia alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa inafufua shirika la uvuvi nchini ili kusimamia shughuli za uvuvi.

"Tunapanga kununua meli za uvuvi ambazo zitakuwa chini ya shilirika hilo la uvuvi na tunatarajia hadi Desemba mwaka huu au Januari mwakani, tutakuwa tumenunua meli ya uvuvi ya kisasa yenye vifaa vyote," alisema.

Alisema kuwa kupitia ufadhili wa nchi ya Japani tayari meli hiyo imeshaanza kujengwa katika nchi ya Srilanka na hadi Januari mwakani wanatarajia kuwa iwe imefika nchini na kuanza kazi. Kadhalika, alisema kuwa Hayati Rais wa awamu ya tano John Magufuli, alikuwa amepanga serikali kununua meli za uvuvi nane kwa ajili ya Zanzibar na Tanzania Bara. Alisema wizara itasimamia kuhakikisha zinanunuliwa meli hizo nane mpya na zenye vifaa vyote kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi na kusafirisha nje ya nchi.

Pia alisema kipaumbele kingine itakuwa ni uboreshaji wa vituo vya uzalishaji wa vifaranga vya samaki ili kuhamasisha jamii kuanza ufugaji wa samaki katika maeneo yao.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema kuwa wameanzisha kampeni ya kuhamasisha jamii kuhusu ufugaji wa samaki na wanatarajia kuweka mashamba darasa katika kila wilaya nchini.

"Pia tunatarajia kufanya upembuzi yakinifu katika maeneo ya bahari na maziwa ili kubaini maeneo ambayo tunaweza kuwapatia wananchi wanaohitaji kufuga samaki katika vizimba kando ya maeneo hayo," alisema Ndaki.

# BAKWATA: Tanzania sasa itapiga hatua

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Mkoa wa Dodoma, limesema kuwa kuchaguliwa kwa Makamu wa Rais Mteule Dk. Philip Mpango, ni mategemeo makubwa kwa Watanzania kuwa nchi sasa itapiga hatua kwa kuwa imeshikwa na viongozi wanaofanana kwenye utendaji wao.

Uteuzi wa Dk. Mpango ulifanyika juzi baada ya jina lake kupendekezwa na Rais Samia Suluhu Hassan na kuthibitishwa na Bunge ambaye hapo awali alikuwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Shekhe wa Mkoa wa Dodoma Mustapha Rajabu, alisema kuwa uteuzi wa Dk. Mpango kuwa Makamu wa Rais ni sahihi kwa kuwa wataifanya kazi kwa umoja na mshikamano kwa malengo ya kuwapatia Watanzania maendeleo.

Shekhe Rajabu, alisema kuwa kutokana na safu hiyo ya juu iliyopo madarakani Watanzania sasa wana imani na mategemeo makubwa, kuwa nchi sasa inaenda kukua kiuchumi ikizingatiwa viongozi hao wana utendaji wenye lengo ya aina moja ya kukuza uchumi.

"Mimi kama kiongozi wa dini ni imani yangu na mategemeo yangu zaidi yapo kwa viongozi hao wa ngazi za juu kwa kuwa wanafanana katika utendaji wao, hivyo nchi sasa inaenda kukua kiuchumi zaidi na watu wake wanaenda kubadilika kimaendelea zaidi," alisema.

Pongezi hizo pia zilienda kwa Chama Cha Mapinduzi kwa kukubali kulipitisha jina hilo na kutambua kuwa Dk. Mpango ana uwezo mkubwa wa kufanya kazi kwa maslahi ya Watanzania wote bila kujali itikadi.

"Mara zote Rais Samia kwa jinsi ninavyomfahamu kwa sehemu kwenye utendaji wake, hafanyi kazi kwa kukurupuka, kwa maana hiyo mpaka kufikia hatua hiyo ya kumteua Dk. Mpango basi tayari amekubaliana na vigezo vya utendaji kazi wake."

"Nimeona sifa za Dk.Mpango zinafanana kabisa na za Rais Samia kwa kuwa wote wamepitia kwenye mazingira magumu, wanazifahamu shida za watu, hawana makuu wala si wabinafsi, hakika watatuvusha," alisema Shekhe Rajabu.

Aliwataka pia Watanzania kuwa na matumaini na uongozi uliopo kwa kuhakikisha upendo, amani na mshikamano vinadumishwa kwa watu wote bila kujali itikadi za kisiasa, kidini na za kikabila.

Shekhe Rajabu pia amesema kuwa katika kipindi hiki ambacho viongozi wote wamepatikana kwa mujibu wa Katiba ya nchi ni vyema wakaheshimiana na kufanya siasa safi huku wakiachana na kuacha chuki za visasi badala yake wakae meza moja na kumaliza tofauti zao.



Wabunge Anne Malecela wa Jimbo la Same Magharibi na Charles Kimei wa Vunjo, wakiingia Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TASAF yawajengea zahanati wakazi Goima

**Na Renatha Msungu,** CHEMBA

WAJAWAZITO katika kijiji cha Igunga, Kata ya Goima, wilayani Chemba mkoani Dodoma, wameondokana na adha ya kutembea umbali wa kilomita saba kwenda kijiji cha Goima kupata huduma ya afya, baada ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF), kuwajengea zahanati.

Kijiji hicho chenye wakazi 3,600, awali walilazimika kutembea umbali wa kilomita saba kuelekea kituo cha afya cha Goima na Hamai kwa ajili ya kupata huduma za afya.

Mwenyetiki wa kijiji cha Igunga, Juma Bakari, alisema hayo juzi wakati wa ziara ya kutembelea wanufaika wa TASAF.

Bakari alisema, kabla ya TASAF kushirikiana na wakazi wa kijiji hicho kujenga zahanati hiyo, wajawazito na wagonjwa wengine walilazimika kupanda bodaboda na wengine kutembea umbali mrefu kwenda kupata matibabu.

"Tumekutana na changamoto kubwa sana ya kutumia pikipiki kusafirisha wajawazito kwa ajili ya kwenda kujifungua, tunaishukuru TASAF kwa kutuwezesha kupata zahanati," alisema Bakari.

Alisema hivi sasa wakazi wa kijiji cha Igunga na vijiji vya jirani wanakuja kupata huduma za afya kutoka katika zahanati hiyo.

Naye muhudumu wa afya wa zahanati ya Igunga, Rehema Daruweshi, alisema kwa siku wanahudumia wagonjwa wa kawaida zaidi ya 15 na wajawazito 10.

Daruweshi, alisema tatizo kubwa waliokuwa nalo ni uhaba wa watumishi katika zahanati hiyo, ikiwamo nyumba za watumishi.

"Naishi mbali na zahanati muda mwingine inaniwia vigumu kutoka usiku kwenda kuhudumia wagonjwa," alisema Daruweshi.

Aliiomba serikali kuwapatia msaada wa kuongeza watumishi pamoja na majengo ya zahanati hiyo.

Sofia Juma, alisema kitendo cha kuleta zanahati Igunga kimepunguza changamoto iliyokuwa ikiwakabili wajawazito ya kutembea umbali mrefu.

Alisema watoto wake amejifungulia katika zahati hiyo jambo ambalo linawafanya kujisikia vizuri kutokana na kusogezewa huduma maeneo ya jamii.

Ofisa Malalamiko Idara ya Mawasiliano TASAF, Makwinja Yusuph, alisema TASAF ina makundi manne ya kusaidia jamii, ambayo hutengewa fedha kwa ajili ya kusaidia kuibua miradi ya kuleta maendeleo kwa jamii husika.

Alisema katika eneo la Igunga waliamua kujenga zahanati ambayo inasaidia watu wa maeneo hayo kupata huduma iliyobora katika kijiji hicho badala ya kwenda kijiji kingine.

"Baada ya kutembelea kijiji hiki TASAF tuliamua kutoa fedha ambapo kamati iliundwa kushirikiana na wanakijiji kuchangia ujenzi wa zahanati hiyo," alisema Makwinja.



# Raia wa China matatani tuhuma kuwapiga madereva

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia raia wa China, Xiao Yong, kwa tuhuma za kuwashushia kipigo Watanzania wawili ambao ni madereva kwenye kampuni ya mchezo wa kubahatisha ya Bonanza baada ya kudai kuwa vijana hao wameiba Sh. 240,000, mali ya kampuni hiyo.Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema polisi walimkamata raia huyo, baada ya kupata taarifa za kuwapo kwa vitendo vya unyanyasaji wa wafanyakazi kwenye kampuni hiyo.

Alisema taarifa hiyo ilianza kusambaa kwenye mitandao ya kijamii ikionyesha raia huyo kuwashushia kipigo na ndio Jeshi la Polisi likaanza kufanya upelelezi na kumkamata.

Alisema Yong anafanya shughuli za michezo ya kubahatisha katika eneo la Mabatini, Kata ya Meta na walimtia nguvuni mtuhumiwa.

"Tulipata taarifa ya kuwapo kwa raia wa kichina kunyanyasa Watanzania kwa kuwacharaza viboko kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii, tulichukua hatua ya

kumkamata mtuhumiwa ambaye alikiri kufanya hivyo kwa madai kuwa wafanyakazi wake ambao ni Watanzania kuiba fedha kiasi cha Sh. 200,000 na kisha kwenda kuvinjari nazo kwenye ufukwe wa Ziwa Nyasa lilipo wilayani Kyela," alisema Matei.

Kutokana na mazingira hayo, Matei alionya wawekezaji wa kigeni kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwa kunyanyasa kwa vipigo au kuwapatia ujira mdogo Watanzania badala yake wazingatie sheria, kanuni na taratibu za nchi.

Katika hatua nyingine, Kamanda Matei alisema jeshi hilo linawashikilia watu watano wote raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kwa tuhuma za kuingia nchini kinyume cha sheria.

Alisema raia hao walikamatwa wakiwa ndani ya basi la Sasebosa linalofanya safari zake kati ya Mbeya, Chunya na Tabora.

Alisema baada ya utaratibu kukamilika watuhumiwa hao, watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

"Hii ni mara ya tano basi la Sassebosa linakamatwa likisafirisha raia wa kigeni,

natoa wito kwa basi hilo kuacha tabia hiyo kabla hatua zaidi za kisheria hazijachukuliwa," alisema Matei.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (wa pili kushoto), akitoa maelekezo kwa viongozi juzi, kuangalia barabara zote zilizopo katikati ya Jiji la Mbeya, zinaruhusu magari ya kwenda na kurudi, kuliko ilivyo sasa ambapo baadhi haziruhusiwi kufanya hivyo. PICHA: GRACE MWAKALINGA

# Waandishi Mbeya wampongeza Makamu wa Rais

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

CHAMA cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya (MBPC), kimempongeza Makamu wa Rais wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, kuteuliwa katika nafasi hiyo na wana imani serikali itaondoa vikwazo vyote vinavyowakabili wanahabari ikiwamo kutopewa ushirikiano kwa baadhi ya watendaji wa taasisi za umma na kutokuwa na uhuru wa kuandika na kuripoti habari zenye maslahi kwa taifa.Akizungumza jana na Nipashe, Makamu Mwenyekiti wa MBPC, Joseph Mwaisango, alisema wanaamini kuwa sasa uhuru wa vyombo vya habari utakuwa mkubwa, watapata ushirikiano kwenye vyanzo mbalimbali vya habari ili kutimiza jukumu lao la kuhabarisha Watanzania.

Alisema anaamini serikali itaendeleza mazuri yaliyoasisi na Hayati Dk. John Magufuli katika kuisaidia Tasnia ya Habari kusonga mbele ikiwamo kuanzishwa kwa sheria mpya ya huduma ya vyombo vya habari ambayo imelenga kuboresha sekta hiyo.

"Tunaungana na Watanzania wote kumpongeza Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan pamoja na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, tunatamani kufanya kazi kwa uhuru na kupewa ushirikiano pale tunapohitaji taarifa mbalimbali nia yetu ni kulisaidia taifa kusonga mbele, tumeshuhudia baadhi ya vyombo vya habari vikichukuliwa hatua mbalimbali ikiwamo kufungiwa au kulipa faini kutokana na sababu mbalimbali najua kwa utawala huu busara na sheria vitatawala zaidi ili kuijenga Tanzania," alisema Mwaisango.

Katika hatua nyingine Mwaisango aliiomba serikali kuendelea kutumia vyama vya waandishi wa habari kutoa elimu ya masuala mbalimbali kwa kuwa wao ni daraja la kufikisha ujumbe kwa wananchi.

Baadhi ya waandishi wa habari mkoani Mbeya akiwamo, Felister Richard, alisema miongoni mwa sababu zinazochangia taarifa kufichwa na vyanzo vya habari ni kuwapo na viashiria vya rushwa, pia maslahi binafsi ya habari zenyewe.

Alisema vyombo vya habari sio mahakama bali kazi yao ni kuripoti au kuandika hali halisi iliyopo ili kuongeza uwajibikaji na wananchi kufahamu mambo yanayoendelea.

Mmoja wa wananchi wa Mkoa huo, Justine Andembwisye, alisema vyombo vya habari ni chombo muhimu kwa ustawi wa taifa na vinahitaji uhuru wa kuripoti na kuandika mambo yote yanayotokea.

Alisema kumeshuhudiwa uhuru wa vyombo vya habari kuminywa au kuzuiliwa kuchukua habari katika baadhi ya maeneo jambo ambalo ni kinyume na Katiba ya nchi ambayo inaeleza kuwa wananchi wanayo haki ya kupata taarifa.

Aliiomba serikali kuboresha mazingira ya utoaji wa taarifa ili kufahamu masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo na uwajibikaji kwa madai kuwa vyombo vya habari wanavitegemea kujua mambo mbalimbali yanayoendelea.

## TARI yakamilisha utafiti kufufua zao la ulezi

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole, mkoani Mbeya imekamilisha utafiti wa kufufua zao la ulezi ambalo linadaiwa kuwa hatarini kutoweka kutokana na uzalishaji wake kupungua nchini.

Licha ya kulimwa kwa kiwango kidogo, zao hilo linaelezwa kuwa na faida kubwa kiuchumi na wataalamu wanasema lina virutubisho vingi kwa afya ya binadamu kuliko mazao mengine ya nafaka.

Ulezi asili yake ni Afrika Mashariki, ambako limekuwa likilimwa kwa miaka mingi, katika miaka ya hivi karibuni kilimo cha ulezi kimeshuka kiasi kikubwa.

Kutokana na zao hilo kuwa katika hatari ya kutoweka, wataalamu wa TARI Kituo cha Uyole wameamua kuchukua hatua za kulinusuru na kuhamasisha kuongeza uzalishaji kwa faida ya wakulima na taifa kwa ujumla.

Akizungumza na Nipashe, Mtafiti Mwandamizi wa mazao ya mpunga na ulezi, Dk. Denis Tippe, alisema ili kulifufua zao hilo sasa wamekuja na mkakati ya kusambaza aina tatu za mbegu ambazo zilitalimwa maeneo yote nchini.

"Zao la ulezi lina faida kubwa kwa afya ya binadamu kuliko mazao mengine ya nafaka, kwa vile lina madini mengi ya Zinc, chuma na virutubisho vingine vinavyopatikana kwa wingi kulikon kwenye mazao mengine ya nafaka," alisema Dk. Tippe.

Alisema Watanzania wamekuwa na jadi ya kutumia ulezi kwa kusaga na kupata unga ambao huutumia kwa kupika uji, ugali, vitafunwa na aina mbalimbali za vilevi, hali ambayo inafanya zao hilo kuwa muhimu zaidi kwa wananchi.

Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema tayari wamekamilisha utafiti huo na kupata aina tatu za mbegu bora za ulezi zenye uwezo wa kutoa mazao mengi na kuleta faida kubwa kwa wakulima wa zao hilo.

Alisema mbegu hizo tayari zimeanza kusambazwa maeneo mbalimbali nchini na kwamba zitapandwa kulingana na aina ya udongo uliopo katika eneo husika, kwa lengo la kuongeza mavuno kutoka gunia sita kwa ekari hadi gunia 40.



# SMZ yakaribisha wawekezaji sekta mbalimbali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema iko tayari kuwakaribisha wawekezaji mbalimbali kuwekeza katika sekta tofauti ili kukuza uchumi wa visiwa hivyo.

Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Ahmed Nassor Mazrui, alisema hayo wakati alipokutana na ugeni wa kampuni ya Afriamco kutoka Emirate, ambayo imekusudia kujenga kiwanda cha kuzalisha dawa za binadamu Zanzibar.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Afya itahakikisha inawapa fursa wawekezaji wanaotaka kuwekeza katika sekta hiyo ya afya ili kuboresha na kuimarisha huduma zinazotolewa. Pia alisema uwekezaji huo utawanufaisha wananchi wa Zanzibar ikiwa ni pamoja na ajira na wanafunzi kupata mafunzo kwa njia ya vitendo vya utengenezaji na upatikanaji wa dawa kwa urahisi.

Meneja mkuu wa Kampuni ya Afriamco, Mhandisi Khalid Mohamed Abubakar, alisema wanashauku kubwa ya kuwekeza kiwanda cha kuzalisha dawa na kutasaidia kupunguza gharama za uagizaji wa dawa kutoka nje ya nchi.

Alisema dawa zitakazozalishwa zitauzwa ndani na nje ya nchi na kurahisisha upatikanaji wa dawa kwa bara la Afrika.

Kampuni ya Afriamco ambayo makazi yake ni Emirate ina uhusiano wa karibu na nchi ya China, India na pia imejikita katika nchi 17 katika bara la Afrika.



Mwenyekiti wa kamati ya kusimamia viongozi wakuu wa kitaifa ya Baraza la Wawakilishi, Khamis Hassan Hafidh, akiongoza wajumbe wa kamati hiyo, kukagua ubora wa baadhi ya milango ambayo inakusudiwa kutumika katika ukumbi wa mitihani katika Shule ya Fujoni, mjini Zanzibar juzi, ni miongoni mwa mradi wa TASAF. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Hospitali kubwa ya kisasa kujengwa Binguni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Ustawi wa Jamii Wazee Jinsia na Watoto Zanzibar imesema imekusudia kujenga Hospitali ya Rufani ya kisasa Binguni ili kuondoa usumbufu na msongamano kwa wananchi katika hospitali kuu ya Mnazi Mmoja.

Akitoa taarifa ya mradi wa utekelezaji wa ujenzi hospitali ya rufani ya kisasa na kufundishia ya Binguni, Mkoa wa Kusini Unguja, Waziri Nassor Ahmed Mazrui, alisema kuwa Zanzibar inahitaji hospitali kubwa ili kupunguza idadi ya wananchi wanaohitaji kupata huduma kwa wakati.

Alisema kuwa azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kujenga hospitali hiyo ni kuhakikisha huduma za matibabu yote zinatolewa nchini bila ya kufuata nje ya nchi.

Pia alisema katika kutekeleza hilo serikali ilitenga eneo lenye ukubwa wa ekari 31.8 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali yenye uwezo wa vitanda 1,000 na kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa kada za afya.

Waziri Mazrui alifafanua kuwa katika uongozi wake aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Muhammed Shein, alitembelea sehemu inayotarajiwa kujengwa na kuagiza kuongezwa kwa eneo hilo na kufikia ekari 65 na kufikiwa hatua ya kujengwa hospitali hiyo ambayo itatoa huduma kwa wagonjwa wanaosafirishwa nje ya nchi.

Alisema katika ujenzi huo kutaanzishwa chuo cha taaluma ya udaktari bingwa chenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,000 kwa wakati mmoja, nyumba za wafanyakazi na mabweni ya wanafunzi.

Kadhalika, alisema serikali inapeleka wafanyakazi wake nje ya nchi kwenda kupata ujuzi zaidi ili kuja kutoa huduma kwa jamii ujenzi huo utakapokamilika na kupunguza tatizo la wataalamu wa maradhi mbalimbali nchini.

"Tunapeleka madaktari wetu nje ya nchi ili kupata ujuzi zaidi kimafunzo na baadaye waje watumikie nchini kwao hivyo lazima wawe wazalendo katika nchi yao," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Omar Dadi Shajak, alisema kuwa serikali ya awamu ya nane inashughulikia ujenzi wa hospitali hiyo ili ionyeshe uhalisia katika jengo hilo.

Ujenzi wa hospitali hiyo umesitishwa baada ya kuona kampuni iliyokusudia kujenga jengo hilo haina uwezo wa kujenga kutokana na ukubwa wake na kwamba wataendelea baada ya kupata kampuni ambayo itakuwa na uwezo.

Aidha, alisema watajitahidi kufanyakazi kwa ushirikiano wa haraka ili kukamilisha ujenzi huo kwa ufanisi zaidi na wanakoelekea ndiko kwenye mafanikio zaidi kwa kuwa maazimio ya serikali lazima yakaguliwe na kufanyiwa kazi ili wafikie malengo.

Kwa upande wao wanakamati wa bajeti ya Baraza la Wawakilishi wametaka kufahamu hatua gani zilifanyika hadi kufikia uamuzi wa ujenzi huo na kampuni gani ambayo itashughulikia hadi kukamilika kwake.

# Watakiwa kumuenzi JPM kwa kufanya maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa kamati ya wazazi shule ya Kama, Mkoa wa Magharibi Unguja wametakiwa kumuenzi aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. John Magufuli kwa kujikita zaidi katika maendeleo ya sekta ya elimu na kuona taifa linapata vijana watakaoongoza baadaye.

Hayo yalisemwa na Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, wakati akizungumza na wazazi wa jimbo hilo baada ya kukabidhi jumla ya matofali 200 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa manne ya Shule ya Kama, Unguja.

Alisema katika kipindi cha uhai wa Dk. Magufuli, alitangaza sekta ya elimu bure kuanzia msingi kwa lengo la kupunguza mzigo kutoka kwa wazazi kulipia gharama za elimu. Aidha, alisema hatua hiyo imekwenda sambamba na upande wa Zanzibar ambayo baada ya Mapinduzi ya Zanzibar tangu mwaka 1964 hadi leo elimu inatolewa bure kuanzia msingi hadi sekondari ili kuwapunguzia mzigo wazazi kulipa gharama za sekta hiyo.

"Wajumbe wa kamati ya wazazi wa shule ya Kama tumepoteza kiongozi wetu shujaa wa taifa la Tanzania...njia pekee ya kumuenzi Dk. Magufuli ni kuhakikisha tunawapeleka watoto wetu kupata elimu ya msingi ambayo kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni bure kama ilivyo Zanzibar na lengo kuona watoto wanasoma na kufaulu kuendelea mbele," alisema.

Aliwataka wazazi pamoja na walimu kuongeza juhudi za kufuatilia maendeleo ya wanafunzi pamoja na kuwa tayari kujitokeza kuchangia maendeleo ya shule ikiwamo michango midogo.

Alisema serikali imefuta ada za masomo kwa wanafunzi, lakini ipo michango ambayo wazazi wanastahiki kuchangia kwa ajili ya kuleta maendeleo na mabadiliko makubwa ya sekta ya elimu.

"Ni kweli serikali imefuta michango ya shule kwa wanafunzi wote kuanzia msingi na sekondari ambapo lengo kuhakikisha wanasoma katika mazingira mazuri ya kuwapunguzia mzigo wazazi...lakini ipo michango midogo midogo sisi wazazi tunalazimika kuchangia," alisema.

Katika hafla hiyo Machano alikabidhi mifuko ya saruji 50 pamoja na matofali 400 na nondo kwa ajili ya ujenzi wa madarasa manne ili kutoa nafasi kwa wanafunzi kusoma vizuri.

Akipokea msaada huo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Kama, Khamis Omar Khamis, alisema wanakabiliwa na tatizo la uhaba wa madarasa na kuwafanya wanafunzi kusoma kwa vipindi vya asubuhi na mchana.

Alisema wamepokea msaada huo ambao matarajio yao kuanza mara moja kwa ujenzi wa madarasa hayo ili kuwawezesha wanafunzi kusoma vizuri kwa wakati mmoja wa asuhuhi pekee.

"Tunakupongeza kwa dhati mwakilishi wa jimbo la Mfenesini kwa kuitikia wito wetu wa mahitaji ya vifaa vya ujenzi wa shule...tunategemea kuanza mara moja ujenzi wa madarasa manne," alisema.

## HABARI KITAIFA

# HAFLA YA KUAPISHWA MAKAMU WA RAIS IKULU YA CHAMWINO MKOANI DODOMA



Dk. Philip Isdor Mpango akitia saini hati ya kiapo, baada ya kuapishwa na Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Hamis Juma kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA ZOTE: IKULU**



Rais Samia Suluhu Hassan akifuatilia hafla ya uapisho.



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi mbalimbali wakati akitangaza majina ya Mawaziri na Manaibu Waziri aliowateua katika Baraza la Mawaziri.



Viongozi mbalimbali waliohudhuria hafla ya uapisho.


**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF FINANCE AND PLANNING**
**GAMING BOARD OF TANZANIA**

GAMING BOARD OF TANZANIA

**TAARIFA KWA UMMA**

**TUKIO LA KUCHAPWA VIBOKO WAFANYAKAZI WA KAMPUNI YA BONANZA**

Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (Gaming Board of Tanzania) imepokea kwa masikitiko taarifa ya tukio lililorushwa kwenye mitandao ya kijamii na vyombo mbalimbali vya Habari mnamo tarehe 31 March, 2021 kuhusiana na kuchapwa viboko kwa wafanyakazi wawili wa Kampuni ya Bonanza na raia wa kichina ambao inasemekana kuwa ni wakuu wao wa kazi.

Tukio hili ambalo limetokea huko Mbeya, ni kinyume cha Sheria na Haki za binadamu. GBT ikiwa ndiyo chombo cha Serikali kinachosimamia na kuratibu uendashaji wa michezo yote ya kubahatisha nchini, tunalifatilia kwa karibu tukio hili ili kuweza kufahamu mazingira halisi ya tukio na hatua za kisheria zinazoweza kuchukuliwa dhidi ya wahusika kwa upande wa Msimamizi wa Sekta.

Hata hivyo, kwa kuwa tukio hili kwa sasa limeshafikishwa Polisi, GBT itatoa ushirikiano unaohitajika ili suala hili liweze kufanyiwa kazi kwa mujibu wa Sheria.

GBT inapenda kuuhakikishia Umma kuwa, itaendelea kusimamia na kuratibu sekta ya michezo ya kubahatisha kwa weledi na kwa kufuata Sheria na Kanuni zilizopo ili iweze kuleta tija katika uchumi wa Taifa letu bila kuleta athari hasi au madhara yoyote kwa jamii yetu.

**Imetolewa na;**
**Mkurugenzi Mkuu**
**BODI YA MICHEZO YA KUBAHATISHA TANZANIA**
**Ghorofa ya 27, PSSSF Twin Towers,**
**Mtaa wa Mission/Sokoine Drive**

**S. L. P 1717 Dar Es Salaam;**
**Simu: 022 2124703/4**
**Tofuti: www.gamingboard.go.tz;**
**Barua pepe: info@gamingboard.go.tz**

# Risasi zarindima jirani na Ikulu Niger

**Niamey,** NIGER

MILIO ya risasi imesikika karibu na eneo la makazi ya rais, ambako pia kuna ofisi ya rais katika mji wa Niamey.

Milio hiyo ilisikika usiku iliyodumu kwa takribani dakika 15, ikifuatiwa na milio ya risasi ya bunduki ndogo, wakazi walisema.

Hali hiyo iliripotiwa baada ya kikosi kutoka kitengo cha Jeshi la Angani, kilicho karibu na Ikulu, kujaribu kuteka makazi hayo ya rais.

Taarifa hiyo ni kwa mujibu wa maofisa wa idara ya usalama nchini humo.

Hali ilisalia kuwa tete na mji huo kwa sasa umewekwa chini ya tahadhari ya hali ya juu.

Ufyatulianaji risasi huo umejiri chini ya saa 48, kabla ya sherehe ya kuapishwa kwa rais mpya mteule, Mohamed Bazoum.

Serikali ya Niger haijatoa tamko lolote kuhusiana na tukio hilo.

Kumeshuhudiwa ongezeko la mashambulio kutoka kwa makundi ya wanamgambo waliojihami, huku taharuki za kisisasa zikikumba nchi hiyo, kufuatia ushindi wa Bazoum katika uchaguzi mkuu wa urais, Februari.

Mpinzani wake rais wa zamani, Mahamane Ousmane, ambaye alishindwa katika duru ya pili ya uchaguzi, alipinga matokeo na kupuuza uamuzi wa mahakama wa kudumisha matokeo hayo.

BBC/VOA



Waandamanaji wanaopinga mapinduzi ya kijeshi nchini Myanmar, wakivikimbia vikosi vya jeshi, mjini Yangon, jana. Zaidi ya watu 500 wanadaiwa kupoteza maisha tangu Februari Mosi, mwaka huu, jeshi lilipochukua madaraka. PICHA: AP

## Kirusi kipya corona chagundulika Israel

**Jerusalem,** ISRAEL

AINA mpya ya virusi vya corona kinachosababisha ugonjwa wa Covid-19, vimegundulika nchini Israel, vinatajwa kuwa ni virusi vinavyobadilika.

Katika taarifa iliyoandikwa na kutolewa na Wizara ya Afya ya Israel, taarifa za kugundulika kwa aina mpya ya virusi hivyo, vinavyobadilika nchini humo zilithibitishwa.

Katika taarifa hiyo, ilielezwa kuwa virusi vinavyozungumziwa vilikuwa vinaambukizwa kwa kiwango kidogo na wala havikusababisha homa kali, hivyo, hakukuwa na sababu ya wasiwasi.

Ilielezwa kuwa chanjo ya Pfizer-BioNTech inayotumiwa Israel pia ni nzuri kwa kujikinga dhidi ya virusi hivyo.

Vyombo vya habari vya ndani ya nchi vilibainisha kuwa virusi hivyo viligundulika kwa mara ya kwanza Novemba, mwaka jana na hadi kufikia sasa viligundulika kwa watu 181.

TRT

## Wakuu wa jeshi wajiuzulu Brazil

**Rio de Janeiro,** BRAZIL

MAKAMANDA watatu wa jeshi wamejiuzulu baada ya Waziri wa Ulinzi kufutwa kazi na Rais Jair Bolsonaro.

Waziri wa Ulinzi, anashukiwa kutaka kulifanya jeshi kuingia kwenye masuala ya kisiasa.

Miaka 57 iliyopita, jeshi lilikuwa likichukua mamlaka nchini Brazil.

Machi 30, katika barua yake ya kujiuzulu, Waziri wa Ulinzi, Jenerali Azevedo alisisitiza umuhimu wa kuliweka jeshi kama taasisi ya serikali.

Ukosoaji ambao wengi wanaona kuwa Rais Bolsonaro anataka kulifanya jeshi kuingilia katika masuala ya siasa.

Bolsonaro hapo awali alitaka kuuawa kwa mkuu wa jeshi la nchi kavu, Jenerali Pujol, ambaye anaunga mkono hatua za kukabiliana na janga la Covid-19.

Aliwafukuza kazi viongozi wa majeshi matatu, ikiwamo jeshi la nchi kavu, anga na majini, kabla hawajajiuzulu.

Bolsonaro anatarajia kutoa ahadi kwa vyama vya mrengo wa kulia, ili kutaka kuendelea kumuunga mkono.

Rais wa Brazil, pia anataka kuhamasisha jeshi kupambana dhidi ya hatua za kukabiliana na janga la corona zilizowekwa katika baadhi ya majimbo.

RFI

# Kaka rais Honduras afungwa maisha jela

**New York,** MAREKANI

TONY Hernandez, kaka wa rais wa sasa wa Honduras, amehukumiwa na mahakama nchini Marekani kifungo cha maisha.

Pia amehukumiwa miaka 30 zaidi, kutokana na biashara ya dawa za kulevya.

Alitakiwa pia kulipa dola milioni 138.5, kiasi ambacho waendesha mashtaka walisema wanachukulia kama ni pesa haramu alizopata kupitia biashara ya dawa ya kulevya.

"Hii ni biashara ya dawa ya kulevya inayofadhiliwa na serikali na hii ndio aina ya tabia ambayo serikali inapaswa kukabiliana nayo.

Kutokana na athari ilivyo kubwa nchini Honduras," alisema mwendesha mashtaka, Matthew Laroche.

Waendesha mashtaka walimshutumu Tony Hernandez, 41, kwa kupokea mamilioni ya dola ya rushwa.

Miongoni mwake ni pamoja na milioni moja kutoka kwa Joaquin Guzman, anayejulikana kama El Chapo, tajiri wa zamani wa kampuni ya Mexico ya Sinaloa.

Fedha hizo, kulingana na waendesha mashtaka wa Marekani, zilisaidia kufadhili kampeni za uchaguzi za chama tawala na kumnufaisha kaka wa Tony Hernandez, ambaye ni Rais wa sasa, Juan Orlando Hernandez.

Juan Orlando Hernandez alikanusha mashtaka hayo. Hajashtakiwa kwa uhalifu wowote.

RFI

## 13 wauawa DRC kwa mapanga

**Kinshasa,** DRC

WATU 13, wameuawa kwa kukatwa vichwa na mapanga, wakati wa mapigano ya kikabila katika Jimbo la Kongo ya Kati, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Waziri wa Afya wa Kasai, Ferdinand Mposhamba, aliwaambia waandishi wa habari jana kwamba, watu tisa walijeruhiwa wakati wa mapigano, ambayo yalitokea katika kijiji cha Bakuakenge kwenye mpaka kati ya majimbo ya Kasai na Kasai ya Kati.

Karibu nyumba 100 na viwanda viwili vilichomwa moto, wakati watu 20,000 wakikimbia eneo hilo.

Mapigano hayo yalisababishwa na tofauti iliyozuka kati ya wananchi wa kabila la Kuba na Lubaphone kuhusu misaada iliyotolewa na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP).

DW

HABARI MICHEZO



# RAIOLA: HAALAND ANAWEZA KUSAJILIWA POPOTE

**DORTMUND, Ujerumani**

WAKALA wa wachezaji, Mino Raiola amedai labda hakuwa makini sana na uhamisho wa Erling Haaland kujiunga na Borussia Dortmund na anahisi nyota huyo anaweza kujiunga na timu yoyote anayoitaka.

Haaland amefanikiwa kujihakikishia kuwa miongoni mwa washambuliaji bora duniani akiwa na umri wa miaka 20, huku klabu za Manchester City, Manchester United, Chelsea, Real Madrid na Barcelona zikiwania huduma ya mchezaji huyo.

Kocha wa United, Ole Gunnar Solkjaer, alimfundisha Haaland katika klabu ya Molde ambapo alifanya vizuri, na alitaka kumsajili ajiunge na mashetani wekundu hao, lakini akajiunga na Dortmund ambapo amefanikiwa kufunga magoli 49 katika michezo 49 aliyocheza.

Maendeleo hayo ya Haaland yamemfanya Raiola kuwaza kuhusu Haaland kujiunga na klabu yoyote duniani, kama angetaka alivyotoka klabu ya Salzburg.

"Kuhusu Haaland, kila mtu alikosea. Amefanya kazi kubwa sana kwa muda mfupi, tofauti na watu wengi walivyotegemea," alisema Raiola akinukuliwa na gazeti la The Athletic.

"Haaland yuko mbele ya ratiba yake na anaweza kujiunga na timu yoyote, aliongeza Raiola.

Raiola ambaye ni wakala wa wachezaji wakubwa duniani kama vile Zlatan Ibrahimovic na Paul Pogba, anaamini kwa sasa Haaland yupo tayari kujiunga na klabu yoyote ile duniani.

## SHAW AJUTIA UTUNDU WAKE ENGLAND



**LONDON, England**

LUKE Shaw amekiri alikuwa hajitoi wala kuonyesha kiwango cha kutosha alipokuwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya England, kinachonolewa na Kocha, Gareth Southgate.

Mlinzi huyo wa kushoto amesema alikuwa akionyesha hali ambayo haikuwa sahihi na alikuwa akiondoka mara kwa mara katika kambi, hali iliyosababisha kuachwa nje ya kikosi cha Simba kwa muda wa miaka miwili.

Baada ya kuwa na umakini na kuimarika katika klabu yake ya Manchester United, Shaw sasa ameitwa tena kwenye kikosi kinachoshiriki michuano ya kufuzu Kombe la Dunia na hataki kuichezea tena nafasi yake hiyo ya pili ndani ya timu ya taifa.

"Nina majuto kadhaa na siwezi kuacha kuwaza kutokana na makosa niliyofanya huko nyuma na hasa na timu ya taifa ya England," alisema Shaw akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilitoroka sana kambini. Kwa kipindi hicho labda sikuwa katika ubora, lakini nadhani miaka miwili iliyopita nimekuwa nikifikiria sana, hayo ndiyo majuto yangu.

"Nikweli nilimwangusha Kocha, Gareth Southagte, sasa najaribu kumzingatia na kumwonyesha kwamba vitu vimebadilika."

## TIMU 36 KUCHEZA LIGI YA MABINGWA ULAYA

**NYON, Uswisi**

BAADA ya majadiliano ya takribani miaka miwili, hatimaye Shirikisho la Soka Ulaya (UEFA), limefikia makubaliano ya kutoa mfumo utakaotumika katika mashindano yake kuanzia mwaka 2024.

Kulikuwa na mvutano wa muda mrefu kuhusu mfumo mpya wa uendeshaji wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na sasa kwenye mfumo mpya, timu 10 zitashiriki mzunguko wa kwanza.

Ushiriki wa timu 10, unapelekea timu zitakazoshiriki mashindano ya Uefa kuanzia mwaka 2024 kuongezeka kutoka timu 32 mpaka 36. Ongezeko hili ni matokeo ya kuondolewa kwa michezo ya makundi na badala yake, kila timu itachuana na timu zingine 10 zinazopishana uwezo.

Sambamba na hilo, mfumo mpya utazipatia timu mbili nafasi ya moja kwa moja.


Timu hizi zitachaguliwa kulingana na uwezo/nafasi ya timu hizo kwenye orodha ya timu zenye mafanikio makubwa kwenye mashindano hayo.

Uteuzi wa timu hizo utategemea kama timu hizo zitakuwa hazijafuzu kushiriki mashindano hayo kulingana na nafasi zilizopo kwenye ligi zao. Kama mfumo huo ungeanza hivi sasa, Liverpool licha ya kuwa kwenye nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, ingefuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao kutokana na nafasi yao kwenye mashindano hayo.

Kwa mfumo mpya, baada ya kila timu kupambana na timu zingine 10, matokeo yatapangwa kwa muundo wa msimamo wa ligi hiyo.

Timu zitakazoshika nafasi nane za juu, zitafuzu kucheza hatua ya mtoano wakati timu itakayoshika kuanzia nafasi ya tisa hadi 24 zitacheza michezo ya kufuzu mashindano hayo.

## HABARI MICHEZO




# WIJNALDUM
## KUPEWA MIAKA MITATU BARCA

**LIVERPOOL, England**

MIAMBA ya Hispania, Barcelona imeripotiwa kumpa ofa ya mkataba wa miaka mitatu kiungo wa Liverpool, Georginio Wijnaldum kama ataungana na klabu hiyo.

Nyota huyo mkataba wake na Liverpool unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na amekuwa akihusishwa zaidi na Barcelona.

Gazeti la Mundo Deportivo limeripoti Barcelona wapo tayari kumpa nyota huyu mwenye umri wa miaka 30 mkataba wa miaka mitatu, ambao utamlipa mshahara wa angalau euro milioni nane kwa msimu.

Wijnaldum naye anatajwa kuwa anatazamia kukubali changamoto mpya mahali pengine, na atakuwa anavutiwa zaidi kufanya kazi na Kocha, Ronald Koeman na kucheza soka nchini Hispania.

Vinara wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Inter Milan pia wameonyesha nia yao ya kuinasa saini ya kiungo huyu, lakini inaaminika kuwa Barcelona ndiyo chaguo la Wijnaldum kama ataamua kuondoka Liverpool.

Wijnaldum ambaye ameshinda Ligi Kuu England na Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Liverpool, amecheza mechi 40 kwenye mashindano yote msimu huu na kufunga mabao matatu.

## UNITED BADO YAKOMAA NA DEMBELE

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United inatajwa kuwa katika mawasiliano ya mara kwa mara na wawakilishi wa Ousmane Dembele kwa ajili ya uwezekano wa kukamilisha dili la kumsajili kipindi cha majira ya joto kinachokuja.



Inaaminiwa kuwa mashetani wekundu hao walishindwa kumpata nyota huyo wa Ufaransa katika dirisha lililopita, baada ya Barcelona kujiondoa kwenye mazungumzo katika dakika za mwisho kuelekea kufungwa kwa dirisha la usajili.

Taarifa zinasema kuwa United walikuwa wanamhitaji nyota huyu kwa mkopo, huku Barcelona wakisimamia msimamo wao wa kutaka kumuuza kwa fedha taslimu.

Kwa mujibu wa taarifa za nchini Hispania, tangu hapo United wamekuwa katika mawasiliano na wakala wa nyota huyu, na sasa wako tayari kuanzisha tena mazungumzo na Barcelona.

Dembele amekuwa akifanya vyema pale Barca kwa simu huu baada ya kutoka kupona majeruhi.

Wakati mkataba wake wa sasa ukiwa umebakiwa na miezi 16, Barcelona wanadaiwa kuwa wanahitaji nyota huyo kubakia klabuni hapo na ikiwa atashindwa kusaini nyongeza ya mkataba basi wataamua kumweka sokoni.

## LEWANDOWSKI KUKOSA MECHI DHIDI YA PSG

**MUNICH, Ujerumani**

ROBERT Lewandowski atakosa mechi zote za robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain, baada ya Bayern Munich kuthibitisha kuwa atakuwa nje ya uwanja kwa muda wa mwezi mmoja kutokana na jeraha la goti.

Lewandowski alipata jeraha la goti lake la kulia wakati wa ushindi wa Poland wa 3-0 dhidi ya Andorra wa kufuzu michuano ya Kombe la Dunia, ambapo alifunga mabao mawili.

Awali ilifikiriwa kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 angepona kwa siku 10, lakini Bayern imethibitisha kuwa majeruhi yake ni makubwa tofauti na ilivyotegemewa.

Taarifa iliwekwa wazi, Lewandowski sasa anatarajiwa kuwa nje ya uwanja wa kwa mwezi mmoja.

"Robert Lewandowski amesumbua mshipa kwenye goti lake la kulia. Mshambuliaji huyu wa Bayern atakuwa nje kwa karibu wiki nne," ilisema taarifa ya klabu ya Bayern Munich.

"Baada ya Poland kushinda 3-0 dhidi ya Andorra, Lewandowski alirudi mapema jijini Munich, ambapo uchunguzi ulifanywa na timu ya matibabu ya mabingwa wa rekodi ya Ujerumani."

Mabingwa hao wa Bundesliga wanakabiliana na wapinzani wao RB Leipzig wikendi hii, kabla ya kukutana na PSG kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kukosekana kwa Lewandowski kutasababisha pengo kwa Bayern kwenye safu ya ushambuliaji, na hiyo inamaana kwamba, Thomas Muller atahamishwa kuchukua nafasi yake au Eric Maxim Choupo-Moting.

## KWA UFUPI

**CITY WAMTAKA KANE**

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27 atakuwa mlengwa wa Manchester City ikiwa viongozi hao wa Ligi Kuu England watashindwa kumsajili mchezaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwishoni mwa msimu huu. (**The Times**)

**CITY, CHELSEA VITANI**

KLABU za Manchester City na Chelsea zipo kwenye mbio moja kuwania saini ya mshambuliaji wa Inter Milan, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 27, raia wa Ubelgiji. (**Eurosport**)

**HAALAND MAWINDONI**

MANCHESTER City ina imani kubwa itafanikisha mpango wake wa kumsajili mshambuliaji wa Norway na Borussia Dortmund, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 20, kama mbadala wa Sergio Aguero. (**Manchester Evening News**)

**GREALISH KUBAKI VILLA**

NAHODHA wa Aston Villa, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 25, huenda akashindwa kujiunga na Manchester City iliyoko chini ya kocha, Pep Guardiola, baada ya klabu hiyo kukatishwa tamaa na ada yake inayotajwa kuwa pauni milioni 100. (**Telegraph**)

**UNITED YAMTAJA AGUERO**

MANCHESTER United imetoa ofa kwa mshambuliaji wa Argentina, Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 32, ambaye ataondoka pale kwenye dimba la Etihad mwishoni mwa msimu huu, huku Chelsea, Inter Milan na Paris St-Germain zikiwa miongoni mwa klabu zinazowania kumsajili. (**Foot Mercato, via Star**)

**LUKAKU ANUKIA BARCA**

BARCELONA inaonekana kama yenye uwezekano mkubwa wa kumsajili Sergio Aguero, ingawa klabu hiyo haijampa kipaumbele badala yake inawafuatilia kwa karibu mshambuliaji wa Lyon raia wa Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 27, Erling Haaland wa Dortmund na Romelu Lukaku wa Inter. (**Mundo Deportivo**)

**MESSI AMTAKA AGUERO**

LIONEL Messi mwenye umri wa miaka 33, ameiambia Barcelona imsajili Sergio Aguero kama sharti mojawapo na yeye kubakia hapo Camp Nou. (**Football Insider**)

**KONATE KUTUA LIVERPOOL**

MLINZI wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Ibrahima Konate mwenye umri wa miaka 21, yupo kwenye nafasi kubwa zaidi ya kujiunga na Liverpool. (**RMC Sport**)

**RODRIGO NJIA MOJA**

NYOTA wa Leeds United ambaye usajili wake ulivunja rekodi, Rodrigo (30), hajaridhika kuendelea katika Uwanja wa Elland Road na huenda akarejea kwenye LaLiga ikiwa ni katika juhudi za kujaribu kujiimarisha kupata tena nafasi katika kikosi cha Hispania. Real Betis na Sevilla zinamnyatia mshambuliaji huyo. (**Fichajes**)

**DE PAUL KUTUA LEEDS**

KIUNGO wa kati wa Argentina, Rodrigo de Paul mwenye umri wa miaka 26, anapania kuhamia Leeds United ikiwa ataondoka klabu ya Udinese ya Italia msimu huu. (**Tutto Atalanta via Teamtalk**)

**WILDER AGOMBEWA**

BURNLEY huenda wakamchukua kocha wa zamani wa Sheffield United, Chris Wilder mwenye umri wa miaka 53, iwapo watamkosa Sean Dyche mwenye umri wa miaka 49, ambaye pia analengwa na Crystal Palace na Newcastle. (**Daily Mail**)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# AGUERO KUJENGEWA SANAMU MAN CITY

### ●●● Bosi wa klabu hiyo afunguka uamuzi huo unatokana na heshima aliyowapa mshambuliaji huyo...

**MANCHESTER,** England

MWENYEKITI wa Manchester City inayoshiriki Ligi Kuu England, Khaldoom Al Mubarak amethibitisha watajenga sanamu ya kumuenzi mshambuliaji wa timu hiyo, Sergio Aguero.

Aguero ambaye ni mfungaji wa wakati wote wa Manchester City atajengewa sanamu hiyo kwa ajili ya kutambua mchango wake kwenye klabu hiyo.

Aguero ambaye amehudumu City kwa misimu 10 mfululizo, anategemewa kutimka klabuni hapo mwishoni mwa msimu ambapo mkataba wake utafikia mwisho.

Nyota huyo raia wa Argentina alitamani kuendelea kusalia klabuni hapo, lakini alifanikiwa kuanza kwenye michezo mitano tu msimu huu kutokana na kusumbuliwa na majeruhi ya goti tangu Juni, mwaka jana.

"Ni heshima kubwa kwetu kuwa na Sergio Aguero hapa, kwa kipindi cha miaka 10 aliyocheza Manchester City ametufanyia makubwa," alisema Al Mubarak akinukuliwa na BBC Sport.

Aguero atakumbukwa kwa kuwa mfungaji bora wa Manchester City akiwa na jumla ya mabao 257 katika michezo 384 aliyocheza.

Nyota huyo alivunja rekodi ya mfungaji wa muda wote wa City, Eric Brooks toka mwaka 2017.

"Misimu 10 nikiwa nimepata mataji makubwa, na kipindi chote nilifanikiwa kuwa mfungaji wa kihistoria wa timu, na kutengeneza uhusiano mzuri na wanaopenda klabu hii - watu ambao watabaki milele moyoni mwangu," aliandika Aguero katika kurasa zake za kijamii.

Kuondoka kwa Aguero kutawalazimu viongozi hao wa Ligi Kuu England kuongeza nguvu katika mbio za kuwania straika wa Borussia Dortmund, Erling Haaland.

HABARI MICHEZO

# NAMUNGO YAIPIGIA HESABU KALI NKANA

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inafanya vyema katika mechi yake inayofuata, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco amesema amekamilisha programu maalumu aliyoandaa kwa ajili ya kuboresha kikosi chake kuelekea mechi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Nkana FC kutoka Zambia.

Namungo FC inatarajia kuwakaribisha Wazambia hao katika mechi ya hatua ya makundi ya michuano hiyo ya kimataifa itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Morocco alisema amepata muda mzuri wa kuwafahamu Nkana FC na tayari amefanyia kazi upungufu wa timu yake kwa ajili ya kukabili wapinzani wao wakiwa imara.

Morocco alisema wachezaji wake wako tayari na mchezo huo na anaamini wataondoka na ushindi wa kwanza kwenye hatua hiyo ya makundi.

Alisema ni mchezo huo ni muhimu kwao kwa sababu ushindi pekee ndio utawarejesha katika matumaini ya kusonga mbele.

"Tunatambua haitakuwa mechi rahisi kwa sababu Nkana FC iko vizuri na wamejipanga, pia tunafahamu katika hatua hii nao hawajapata matokeo kama sisi, tunajua watakuja kusaka matokeo kama ilivyo upande wetu."

"Nina matumaini makubwa ya kufanya vizuri kwenye mchezo dhidi ya Nkana kwa kuhakikisha tunacheza kwa nidhamu ya hali ya juu ili kutafuta matokeo chanya," alisema Morocco.

Aliongeza wanatarajia kumpokea golikipa wao namba moja, Jonathan Nahimana leo akitokea Morocco alipokuwa na kikosi cha Timu ya Taifa ya Burundi ambayo ilichapa bao 1-0 na kupoteza nafasi ya kushiriki katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), zitakazochezwa nchini Cameroon mwakani.

"Mipango inaendelea vizuri, tumeshaona tulipokosea, tunahitaji matokeo chanya katika mechi hii ya nyumbani, hatujakata tamaa ya kusonga mbele, lolote linaweza kutokea katika michezo iliyobakia," Morocco alisema.

Baada ya mechi hiyo, Namungo FC itaikaribisha Ihefu FC kutoka Mbeya katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Aprili 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kassim Majaliwa uliopo mkoani Lindi.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ufukweni wakiwa katika picha ya pamoja kabla ya kuanza kwa mechi ya kwanza ya kuwania tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON- Beach Soccer), dhidi ya Burundi iliyochezwa kwenye ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam juzi. Tanzania ilishinda mabao 8-3. **PICHA: TFF**

# Kiwango Ufukweni chamkera Pawasa

**Na Saada Akida**

LICHA ya kupata ushindi mnono wa mabao 8-3 dhidi ya Burundi, Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ufukweni, Boniface Pawassa amesema hajaridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mchezo huo wa kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa Afrika uliochezwa juzi.

Timu hizo zitarudiana Jumamosi kwenye Ufukwe wa Coco na mshindi atafuzu kucheza fainali hizo zitakazochezwa Mei, mwaka huu nchini Senegal.

Pawasa alisema kikosi chake kina uzoefu na mashindano hayo lakini hawakucheza katika kiwango chao kilichozoeleka.

"Tulihitaji kumaliza mchezo huu ili tutakaporudiana iwe kazi nyepesi na kuanza maandalizi ya kwa ajili ya safari yetu ya kwenda Senegal kwa ajili ya kucheza fainali hizo, ila nina mshukuru Mungu tumemaliza salama mchezo huo," alisema Pawasa.

Aliongeza kikosi chake kinatakiwa kujiimarisha zaidi kwa sababu wapinzani wao wana kikosi imara na wanaweza kupindua matokeo.

Naye Kocha Mkuu wa Burundi, Bulenge Ally alitaja sababu mojawapo iliyopelekea kupoteza mechi hiyo ni kuondolewa na nyota wake wanne baada ya kugundulika kuwa na virusi vya COVID-19 na kushindwa kucheza mechi hiyo.

"Wachezaji hao walikuwa katika sehemu ya mipango yangu ya mchezo huu, lakini kabla ya mechi tukaambiwa hatuwezi kuwatumia, jambo hili lilishusha morali ya wachezaji wengine pamoja na benchi lote la ufundi," alisema Bulenge.

## Yanga Princess matumaini kibao

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, amesema hana hofu ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu huu licha ya wapinzani wao, Simba Queens kuongoza katika msimamo wa ligi hiyo.

Edna aliliambia gazeti hili kikosi chake kitaendelea kupambana kuhakikisha wanafanya vizuri katika kila mechi ili kurejea katika nafasi ya uongozi wa ligi hiyo kama ilivyokuwa wakati wa mzunguko wa kwanza.

Kocha huyo alisema hadi sasa hakuna timu ambayo ina uhakika wa kutwaa ubingwa huo na alizitaja timu nyingine zilizoko katika nafasi ya kushinda taji hilo ni mabingwa watetezi, Simba Queens na JKT Queens.

"Kuna timu tatu ambapo mojawapo inaweza kuchukua ubingwa huo na itafanikiwa kuzichanga vizuri karata zake," alisema kocha huyo.

Alisema katika mechi tano zilizobakia ana imani ataondoka na ushindi na hivyo atajiimarisha kwenye mbio za kuwania ubingwa wa msimu huu kama ambavyo malengo yake yalivyokuwa.

"Kuhusu ubingwa ni suala la kila kocha kuzichanga karata zake, kwangu nina imani ya kufanya vizuri katika michezo mitano ambayo tutakuja kumalizia, na kufikia kile ambacho kinatarajiwa na wanayanga," alisema Edna.

## Zimamoto nguvu zote Kombe la FA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kupoteza matumaini ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu, Kocha Mkuu wa Zimamoto, Mohamed Ali Hilali "Teddy" amesema nguvu zake zote anazihamishia katika mashindano ya Kombe la FA.

Akizungumza na gazeti hili jana, Teddy alisema amekubali kikosi chake kimejiondoa kwenye mbio za ubingwa wa ligi baada ya kupata matokeo ya 'kelgalega', hivyo wanajiimarisha kusaka matokeo chanya kwenye michuano ya FA.

Teddy alisema katika kuhakikisha lengo lao linatimia, tayari kikosi chake kimeshaanza mazoezi kwa lengo la kukabiliana na ushindani katika mechi yao inayofuata dhidi ya Kilimani City inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza.

"Macho yetu na akili zetu kwa sasa tumezielekeza katika Kombe la FA, lakini hata katika michezo ya ligi hatujapoteza matumaini sana kwa kuwa kwenye soka lolote linaweza kutokea," Teddy alisema.


Aliitaja Kilimani City kutoka Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja kuwa ni moja ya timu zenye wachezaji wazuri na hiyo inatokana na kusajili nyota vijana.

Bingwa wa michuano ya Kombe la FA hupata tiketi ya kuiwakilisha Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# Michezo

Alhamisi Aprili 1, 2021

Nipashe

## AGUERO KUJENGEWA SANAMU CITY

HABARI UK 22



Mshambuliaji wa Yanga, Yacouba Sogne (kulia), akijaribu kumiliki mpira katika mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kujiandaa na mechi za lala salama ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kurejea tena kuanzia Aprili 8, mwaka huu. Kushoto ni Michael Sarpong. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA SC, YANGA KURUDIANA MEI 8

●●●Ni mechi nyingine muhimu itakayotoa picha ya mbio za ubingwa msimu huu baada...

**Na Mwandishi Wetu**

PAMBANO la marudiano la Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya watani wa jadi nchini, Simba na Yanga limepangwa kufanyika ifikapo Mei 8, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Awali mechi hiyo ilipangwa kuchezwa Machi 8, mwaka huu, lakini iliahirishwa kwa sababu ya ratiba ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo mabingwa watetezi, Simba wanashiriki.

Katika mchezo wa kwanza uliofanyika Novemba 7, mwaka jana, timu hizo ziligawana pointi, Yanga ikitangulia kufunga kupitia kwa Michael Sarpong kwa penalti na beki wa kimataifa wa Simba kutoka Kenya, Joash Onyango aliisawazishia timu yake kwa kichwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), Almasi Kasongo, alisema ratiba mpya iliyotolewa jana imezingatia mashindano yote ya kimataifa ya ngazi ya klabu na Timu za Taifa, Kombe la FA na itamalizika ifikapo Julai 11, mwaka huu badala ya Mei kama ilivyokuwa awali.

"Ukitazama ratiba yetu ile ya awali ambayo tuliitoa kwa vilabu ilikuwa inaonyesha kwamba tarehe 3 na 4 Aprili kutakuwa na michezo ya Kombe la Shirikisho, tarehe 6 hadi 8 Aprili tulikuwa tunarejea kwenye mechi za ligi.

"Kutokana na msiba tafsiri yake ni kwamba ile michezo ya Kombe la Shirikisho na ile ya ligi nayo inakuwa haipo kwa sababu tupo kwenye maombolezo ya siku 21. Kumbuka kwamba siku 21 zinaisha tarehe 7 ambapo kulikuwa na mchezo wa ligi, tarehe 6 kulikuwa na mchezo wa ligi na tarehe 3-4 kulikuwa na mchezo wa Kombe la Shirikisho," alisema Kasongo.

Alisema pia mechi nyingine zilizopangiwa tarehe ni za 'viporo' ambazo zinahusisha timu za Simba, Namungo FC pamoja na Gwambina. Aliongeza mechi za mtoano ambazo zitazikutanisha timu za Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya klabu za Ligi Daraja la Kwanza zitachezwa Julai 14, mwaka huu na watarudiana Julai 17, huku Fainali ya Kombe la FA ikipangwa kufanyika Julai 18, mwaka huu mkoani Kigoma.

Alizitaja mechi za kwanza za viporo zitachezwa Aprili 13, mwaka huu kati ya Biashara United dhidi ya Coastal Union na siku inayofuata Simba itawakaribisha Mtibwa Sugar huku Namungo wakiwafuata Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi Aprili 15, mwaka huu.

Mechi za funga pazia la msimu huu zitachezwa Julai 11 ambapo Simba itawakaribisha Namungo, Yanga itacheza ugenini dhidi ya Dodoma Jiji, Ruvu Shooting itawakabili Azam FC, Mbeya City vs Biashara United, JKT Tanzania vs Mtibwa Sugar, Tanzania Prisons vs Gwambina, Coastal Union vs Kagera Sugar na KMC itawaalika Ihefu. Mpaka sasa hesabu zinazonyesha bado hakuna timu yenye uhakika wa kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na klabu zitakazoshuka daraja wakati zinaelekea kuingia kwenye mzunguko wa 25 kati ya mizunguko 34 ambayo itachezwa msimu huu.

Yanga yenye pointi 50 ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na Simba yenye pointi 46, lakini ikicheza mechi tatu pungufu huku timu tatu zinazoburuza mkia katika msimamo ni Mbeya City, Ihefu zote za jijini Mbeya na Mwadui FC ya mkoani Shinyanga.

## GOMES KUFUNGA HESABU JUMAMOSI

**Na Saada Akida**

ILI kujiweka katika nafasi salama ya kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes amesema anahitaji 'kufunga hesabu' zake katika mechi dhidi ya AS Vita kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Simba yenye pointi 10 na inayoongoza Kundi A inahitaji pointi moja ili kusonga mbele katika mashindano hayo, ikibakiwa na mechi nyingine ya ugenini dhidi ya Al Ahly itakayochezwa hivi karibuni jijini Cairo.

Gomes aliliambia gazeti hili ni muhimu kupata ushindi katika mchezo huo ili kujipunguzia presha katika mechi ya mwisho ya hatua hiyo ya makundi dhidi ya mabingwa wa zamani wa mashindano hayo.

Alisema wamejipanga kuhakikishia wanacheza hatua ya robo fainali kwa kupata ushindi dhidi ya AS Vita ili kufikisha pointi 13 ambazo hazitaweza kufikiwa na Al Ahly inayoshika katika nafasi ya pili ikiwa na pointi saba endapo itashinda michezo yake miwili iliyobakia.

"Mara kwa mara nawaeleza wachezaji wangu kuhusu umuhimu wa mechi dhidi ya AS Vita, tunatakiwa tuhakikishe tunapata ushindi ili kujiimarisha katika nafasi tuliyokuwapo kwa sababu tukipoteza hapa nyumbani, mechi ya mwisho haitakuwa rahisi kushinda ugenini dhidi ya Al Ahly, licha katika soka lolote linaweza kutokea," alisema Gomes. Naye golikipa chaguo la kwanza la Simba, Aishi Manula alisema wanatambua umuhimu wa mchezo huo ambao utakuwa na ushindani mkubwa kutokana na kuwafunga wapinzani wao kwenye mechi ya kwanza walipokuwa ugenini Kinshasa.

"Kocha Gomes ametueleza na wachezaji wote tunajua kwamba utakuwa mchezo mgumu, kwa sababu kama sisi tuliweza kushinda kwao, hata wao wanaweza kufanikiwa kupata matokeo chanya, tutaingia kupambana na hatutaki kuwa njia," alisema Manula.

Wachezaji wa Simba waliokuwa katika timu ya Taifa (Taifa Stars), juzi waliripoti kwenye mazoezi ya klabu hiyo yanayoendelea kwenye Uwanja wa Mo Arena ulioko eneo la Bunju na kukifanya kikosi kikamilike.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002